# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## Verbatim Report of

## DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, GANZE CONSTITUENCY, HELD AT

## GANZE PRIMARY SCHOOL

**ON**

**OCTOBER 8TH, 2002**

**CONSTITUITON OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, GANZE CONSTITUENCY HELD AT GANZE PRIMARY SCHOOL ON 08/10/2002**

**Present:**

Com. Swazuri.

**Secretariat Staff in Attendance**

Lydia Moraa - Verbatim Recorder

Wale ambao wanahudhuria mkutano huu ambao ni muhimu sana kwetu, tunataka tuuanzishe rasmi kwa maombi ambayo yataongozwa na Rev. kutoka sehemu ya Jaribuni. Kwa hivyo Reverend tuongoze kwa maombi.

**Rev. Emmanuel N. Charo:** Na tuombe. Baba yetu unayeishi na kutawala, tunajua ya kwamba yote ambayo inatendeka katika dunia hii ni mipangilio yako, na hata uliona ni vyema siku ya leo ukaichagua ili Bwana shughuli ile ambayo tuko nayo ikaweze kutekelezeka. Tunakurudishia shukurani kwa kuwaleta kwa hali ya usalama kwa wale wote ambao wanahusika, Mungu wa mapenzi tunapoanza shughuli hii tunaikabidhi mikononi mwako ili baba tukaweze kuona ya kwamba yale yote ambayo yataenda kutendeka mahali hapa, yakaweze kuwa na manufaa kwa kizazi hiki na hata vizazi vingi vijavyo. Mungu wa mapenzi katupe amani, na Mungu wetu tuonapo mwisho wa shughuli hii tuzidi kukurudishia shukurani na asante. Bwana tunaomba tukipitia kwa jina la mwanao Yesu Kristo aliye Bwana na Mwokozi wetu tumeomba.

**Speaker:** Asante.

**Chief Anderson Pembe Kahindi:** Mimi ambaye nimesimama hapa kama chief wa hapa Ganze Location, wageni wote ambao wamefika wa Commission, wenyeji wote waliofika kwa mkutano huu ambao ni muhimu kwetu namkaribisha nyote hapa Ganze ambao tuko hapa Ganze Primary School kwa shughuli hii. Kwa hivyo nyote mjisikie mko huru, msikize kwa makini yote ambayo yameletwa na commissioners kuhusu yale ambayo tulikuwa tumeyatoa kama pendekezo. Karibuni sana. Na pia kuna Coordinator wetu hapa Bwana Daniel Maringa atakuwa na machache ya kuzungumzia kabla ya kuendelea na mkutano huu muhimu. Karibu Bwana Daniel Maringa.

**Daniel Maringa:** Asante sana bwana Chief na Commissioner wetu na wengine kutoka Tume ya Marekebisha ya Katiba, wanakamati wa CCC. Nimefurahi sana kuwa hapa. *Haya mlamukadze nyosi.*

**Audience:** *Salama*

**Daniel Maringa:** Salama. Saa sisi leo tuko hapa, nafikiri tumekuwa tukikutana mara kwa mara mnakumbuka tumekuja sana hapa Ganze kwa mambo haya ya Katiba, si ndio hivyo?

**Audience:** Ndiyo.

**Daniel Maringa:** Sasa leo hatukuja na mengine. Tumekuja na yale yale isipokuwa sasa tunataka kuwajulisha ile stage ama ile sehemu ambayo tumefika katika kazi yetu hii ya kurekebisha Katiba. Lakini kabla sijawaelezea ningetaka kuwajulisha ni akina nani ambao tumekuja nao hapa. Nataka kumjulisha kwenu Commissioner wetu Dr. Mohammed Swazuri, ndio huyu Commissioner wetu tafadhali waonyeshe mkono. Yeye ni Commissioner ambaye atakuja awazungumzie nitawaeleza kwa machache kidogo. Tuko na recorder wetu pale ambaye ametoka pia Nairobi kule ni Noor Awadh. Yale yote yatakayosemwa hapa yeye atayaandika kwa maandishi ili yajulikane tulikuwa kule Ganze na ni kitu gani kilichozungumzwa. Na hapa vile vile mnaona huyu ananukua na sauti. Maanake yule anaandika na huyu vile vile ananukua na sauti ili iwe hakikisho kwamba hayo ndio yaliozungumzwa. Anaitwa Lydia Moraa.

Nafikiri mnamfahamu CCC wetu ambaye ni hapa hapa Councilor Susan Biria, ndio huyo pia yeye anashughulika na mambo haya tumekuwa tukipanga mikutano mingi kwa mambo haya haya. Sasa nafikiri sitapoteza mda mrefu nataka tu niwaeleze kwa kifupi kwamba tulikuja hapa tukazungunza machache kuhusu marekebisho ya Katiba, tukasema tutarudi ili tuje tuchukue maoni yenu na kwa hakika tulifanya hivyo. Si mlikuja mkatoa maoni? Basi Tume ya Marekebisho ilichukua maoni yenu, ikaketi mwezi mzima, kule Mombasa wakazungumzia yale yote mlikuwa mmeyasema, yakachukuliwa kwa pamoja na kukatolewa huu mswada ambao Daktari wetu Commissioner Mohammed Swazuri atayazungumzia kwa kirefu, awaeleze ni yapi yaliozungumzwa na ni yapi yaliopendekezwa na mapendekezo yale yako vipi na hiyo Katiba mpya iko vipi, na kile nataka

tufahamiane ni kwamba hii sio Katiba.

Hatuna Katiba kwa sasa, hili ni pendekezo tu kulingana na yale mapendekezo yaliochukuliwa kutoka sehemu ya uwakilishaji bungeni maeneo mia mbili na kumi. Baada ya hapa, tutakuwa na kongamano la kitaifa yaani National Constitutional Conference ambapo pale kutakuwa na waakilishi wa sehemu mbali mbali. Katika kila wilaya kuna watu watatu ambao tayari tushafanya uchaguzi. Nafikiri Councillor Susan Biri alikuwepo. Hao ndio waliochagua kwa hivyo kusema kwamba ilikuwa hivi na vile. Ilikuwa ni uchaguzi ambao ulifanywa kwa halali na wazi kabisa. Tukapata watatu ambao watakwenda kule Nairobi ili kuzungumzia jambo hili kutuwakilisha. Kutakuwa vile vile na watu wengine kama vile wabunge watakuweko, kutakuwa na watu arobaini kutona zana mbali mbali za kisiasa, kutakuwa na watu mia moja na ishirini na tano kutoka makundi tofauti kama vile professional bodies, disabled, vyama vya dini na wengineo ili mradi tupate kongamano nafikiri zaidi ama kukaribiana na mia sita ishirini na tano hivi au mia saba. Kwa hivyo kwa leo hatutazungumza mengi.

Nitamkaribisha Commissioner wetu apate kutueleza wengine mmepata mswada ambao tunataka tuujadilie, na ningetaka kuwajulisha ya kwamba huu sio mwisho. Commissioner wetu atafanya official launch ya hii document ama huu mswada lakini sisi, nikizungumza na CC wetu tutapanga pengine mikutano mingine ambapo sasa tuje tujadiliane. Kwa kirefu tutashinda hapa siku nzima kusema hili twalitaka ile hatutaki ili wale watakwenda kutuwakilisha waweze kuwakilisha ya ambayo tunaona sisi kama watu wa sehemu hii ya Ganze na Kilifi nzima kwa jumla, tungetaka yawe ndio mapendekezo yetu. Ama sivyo hivyo? Maanake nataka muelewe kwamba hii tulisema ni process ya wananchi wenyewe, sio process ya mtu. Ni process ya mimi na wewe, akina mama wote mpaka watoto. Kwa hivyo ni sisi tutasema vile wenyewe tunavyotaka kwa hivyo hili ni pendekezo na katika pendekezo tutazidi kuchambua kusema hili hapana, hili linafaa. Au maswali, je mmesema katika mswada wenu kutakuwa na kadhaa kadhaa, je yatatekelezwa vipi? Kwa hivyo leo baada ya Commissioner wetu mwe huru kabisa kuuliza pale ambapo hapaeleweki na mueleze mueze kuelewa kwa nini jambo fulani litakuwa hivi na litafanywa vipi? Mmesema tu kwamba kutakuwa na hivi, je, itatekelezwa vipi? Sawa sawa. Kwa hivyo sikizeni halafu maswali yatakuja. Asante sana. Commissioner wetu tafadhali karibu.

**Com. Mohammed Swazuri:** Habari za asubuhi wazee na akina mama?

**Audience:** Salama.

**Com. Mohammed Swazuri:** Nimefurahi kwamba tumefika hapa leo kama tulivyoahidi kama Coordinator alivyosema, tuliahidi siku ya kwanza tulipokuja hapa tukawa kule Polytechnic mwaka jana, tukaahidi kwamba tutafanya civic education halafu tuje tukusanye maoni, tuandike mswada halafu tuurudishe kwenu kama alivyosema Bwana Mwaringa sasa ndio tumekuja kuurudisha kwenu. Kwa hivyo tumekuja kuwaonyesha ile Katiba ule mswada ambao mwisho utakuwa Katiba ambao mmekuwa mkiushughulikia ndio huu. Halafu tuwaeleze kwa kifupi unasema nini. Kuna wale ambao wanaweza kusoma na kuna wale ambao hawawezi kusoma. Tuwaeleze vizuri kwa ufupi unasema nini, mtapata nafasi kama alivyosema Coordinator

ya kuuzungumzia kwa kirefu baada ya leo, halafu pia tungetaka kupata tena maoni yenu. Ikiwa kuna sehemu ambayo mnafikiria haiko sawa au haiwaridhishi au haimo ilitolewa au ilisahauliwa sasa mtakuwa na nafasi tena ya kutueleza kwamba kipengele fulani tulikuwa tunataka hivi mbona kimekuwa hivi na kadhalika. Bado uwanja ni wenu, bado nafasi ni yenu mueleze. Baada ya kuuangalia huu mswada sasa ndio tutajua na maoni yenu tutatuja kuwa tutaupeleka kwenye mkutano wa kitaifa na ukifika kule utakuwa una sura gani. Kwa sababu tulisema tunarekebisha Katiba, ni vizuri kuwaelezea ile Katiba iliyoko sasa na hii Katiba ambayo tunaipendekeza, kuna tofauti gani. Hapo ndio tutajua kama tumerekebisha au tumetengeneza upya. Halafu baada ya kueleza zile tofauti kubwa zilizoko baina ya Katiba hii ya sasa na hii tunayotaka kuitengeneza ndio tutaenda sasa kwa undani zaidi kifungu kwa kifungu halafu ndio tupatie nafasi watu waeleze au waulize au waseme vile wanavyofikiria ingekuwa lakini haikuwa.

Kwanza Katiba hii mpya ambayo tunapendekeza imetumia lugha ambayo ni rahisi kinyume na ile Katiba ya zamani au ya sasa tunayotumia. Ile lugha ya kisheria ngumu ngumu tumejaribu kuiondoa na tunaendelea kuipunguza.

Halafu pili pia tutaifanya hii Katiba iwe katika lugha ya Kiswahili. Kwa sababu ya ukosefu wa wakati, hatukuweza kuwangojea wale watu wa kutafsiri wamalize lakini wako wanafanya na ikipatikana ile ya Kiswahili italetwa kwenu.

Halafu tofauti kubwa nyingine ni kwamba Katiba hii mmeitengeneza nyinyi wananchi. Ile Katiba ya zamani ilitengenezwa na watu kidogo lakini hii imezunguka Kenya nzima, na tukapata maoni ya watu wengi wa Kenya, tukayachambua ndio tukapata Katiba hii. Kwa hivyo maneno yalioandikwa hapa si maneno ya watu wachache au mtu mmoja au kundi fulani, ni maneno ya wananchi tabaka mbali mbali ya waKenya, hio ni tofauti kubwa na ile Katiba ya sasa.

Halafu Katiba hii iko na utangulizi. Nikikumbuka ile Katiba ya zamani haina utangulizi inaanza moja kwa moja lakini Katiba ya sasa ina utangulizi yaani preamble.

Halafu Katiba ya sasa imezingatia sana masilahi ha mwananchi wa kawaida. Imeangalia sana mambo mwananchi wa kawaida. Maisha yake, uhuru wake, mahitaji yake, yote yamezingatiwa hapa kinyume na Katiba ile ya zamani ambayo haikutia maanani sana mambo hayo.

Halafu humman rights, haki za binadamu. Na haki za kimsingi sasa zimeelezwa wazi wazi ni zipi, zitatekelezwa vipi, zitatekelezwa na nani. Hadhari yake mtu asipotekeleza atafanywa nini. Hizo zimewekwa wazi kabisa na tena ndizo tena zimechukua sehemu kubwa ya hii Katiba. Karibu Katiba nusu ya zaidi ya Katiba yote inazungumzia hayo mambo ya humman rights kwa sababu ni sehemu ambayo wananchi wa Kenya wamelalamika kwamba walikuwa wakipunjwa sana.

Halafu tofauti nyingine bunge sasa litakuwa na sehemu mbili. Tutakuwa na bunge na wakilishi na bunge la kawaida lile la wale wabunge wetu tunaowachagua wale mia mbili na kumi. Halafu kutakuwa na bunge la wakilishi. Kwa hivyo kutakuwa na

Upper House na Lower House ambapo Katiba hii ya sasa haina.

Halafu tofauti nyingine tumelipatia bunge, mabunge yote mawili hayo, tumeyatapia nguvu zaidi. Nguvu tumezitoa kutoka kwa ofisi ya Rais, tumezisambaza katika sehemu hizo. Either bunge la Upper House au bunge la Lower House halafu pia na nguvu nyingine tumezipeleka kwa waziri mkuu. Hiyo ni tofauti nyingine Katiba ya sasa ya Kenya tunayoishia sasa haina cheo cha waziri mkuu. Hii cheo tunayopendekeza tumeweka cheo cha waziri mkuu ambaye pamoja na yale mabunge mawili na mawaziri, watakuwa wanagawana powers ambazo wananchi wa Kenya walilalamika sana kwamba zote ziko katika ofisi moja.

Halafu pia hapo hapo tofauti moja tumesema anayetaka kugombea kiti cha ubunge au cha udiwani au cha uraisi sio lazima awe anatoka kwenye chama. Anaweza kuwa independent candidate. Hiyo ni tofauti kubwa. Kama umeshindwa kupata tikiti ya chama kingine au kimoja unaweza ukasimama wewe mwenyewe kibinafsi ukataka kura.

Pia tumesema kwamba vyama vya kisiasa sasa tumeweka ratiba maalum, tumeweka sheria maalum za kusema vyama vya kisiasa vinatakikana vifanye kazi gani, kazi zao tumeziandika katika Katiba ambazo sasa hakuna katika Katiba ya sasa. Tumeandika sheria ambazo vyama vya kisiasa vitafuata, nani atavisajili vyama sya siasa, nani aweza kuvivunja vyama vya kisiasa. Na pia tumesema vyama vya kisiasa vile ambavyo vina nguvu na vina viti katika bunge, vitapata pesa sasa kutoka kwa serikali.

Jambo jingine la muhimu ni kwamba wabunge na macouncillor, madiwani hawataweza kuamua mishahara yao. Watu walilalamika kwamba wabunge hukaa wakateta lakini ikifika wakati wa kuongeza mishahara wanaungana dakika kumi, wanapitisha mishahara yao. Tumeondoa, wananchi ndio ambao wataamua kupitia kwa vyombo ambavyo tumevitaja hapa mshahara wa diwani, mshahara wa bunge utakuwa ni pesa ngapi. Tena mishahara ya wale wafanyi kazi wa umma wote tumetengeneza tume maalum ya kuchunguza mishara ya watu hawa.

Halafu pia tofauti kubwa tumeweka tumesema ikiwa wananchi hawana imani na mbunge wao au kiongozi wao au Rais au waziri mkuu, wanaweza kumtoa. Hilo lilikuwa ni lalamiko ambalo wananchi walisema na tumeisikia na ni tofauti moja kubwa kati ya Katiba ya sasa na hii tunayoipendekeza.

Bali na hivyo pia tumeweka sheria ya kuhakikisha kwamba viongozi wote wa umma wanafuata sheria fulani. Katika kufanya kazi zao. Leadership code, ethics code. Na tumeweka tume maalum ya kuangalia tu kuchunguza viongozi wanaendesha kazi zao namna gani ili kuondoa mambo ya corruption, mambo ya wizi. Na hiyo akivunja kiongozi akivunja sheria hiyo ni njia moja ni sababu moja ya kutaka kuweza kumtoa katika cheo kile.

Halafu tumesema tofauti nyingine ni kwamba Rais atakayechaguliwa ni lazima apate asilimia hamsini au zaidi ya kura zote. Halafu apate asilimia ishirini katika kila mikoa nusu ya ile mikoa yetu tuliyo nayo. Kama ni mikoa minane awe zaidi ya nusu,

kama ni mikoa mitano awe na twenty percent katika kila mkoa. Tumeweka hivyo kwa sababu pengine mikoa huenda ikaongezwa hapo mbele, bado sheria itakuwa ni ile ile lazima iwe zaidi ya nusu ya idadi ya mikoa tuliyo nayo.

Na kama nilivyosema mwanzo nguzu za Rais tumezipunguza, hatukuziondoa kwa sababu huyu ni kiongozi ya nchi, lakini kinyume na Katiba ile iliyoko nguvu za Rais tumezipunguza na tumezieleza kazi zake na nini. Na kazi za makamu wa Rais pia tumezisema ni zipi. Kazi za waziri mkuu tumezisema, kazi za manaibu tumezisema wazi wazi.

Halafu tumeeleza pia tofauti nyingine kwamba serikali itaongozwa na waziri mkuu. Huyu ndiye atakuwa mkubwa wa shughuli za serikali katika bunge. Na atatoka katika chama kile ambacho kimepata viti vingi zaidi katika bunge.

Halafu tumesema pia Rais ama waziri mkuu anaweza kushtakiwa ikiwa atafanya makosa katika kazi yake. Hiyo ni tofauti ambayo haiko katika Katiba ya sasa.

Halafu tumesema mawaziri hawatakuwa wabunge. Waziri yoyote wa wizara ya serikali atakuwa si mbunge. Watakuwa ni watu tofauti, nje ya bunge, watachaguliwa nje ya bunge. Na tukasisitiza kwamba waziri lazima awe ni mtu ambaye ametaalimika katika ile wizara yake. Waziri wa elimu awe ni mwalimu, mtu ambaye amefanya kazi ya uwalimu. Sio mtu ambaye amefanya course nyingine awe waziri wa elimu.

Halafu tukasema serikali ya umoja, unitary state sasa tumeitoa nguvu zake. Serikali imeenda mashinani sasa. Tunaenda kwa tuna serikali ya kitaifa, central government, tuna serikali ya majimbo ya mkoa, provincial government, tuna serikali ya wilaya, district, tuna serikali ya location na tuna serikali ya kijiji. Hiyo ni tofauti kubwa kabisa kwanza ndio ni kubwa kabisa. Tumeweka serikali tofauti tofauti wananchi wenyewe wataamua nani atawaongoza.

Halafu upande wa mahakama tumeweka supreme court. Baada ya tumeweka court za kawaida hizi, mahakama halafu kuna high court halafu watu walilalamika kwamba baada ya high court hawajui waende wapi. Sasa tumeweka kiwango cha juu zaidi, supreme court. Unaweza ukafanya appeal au ukafika huko kwa supreme court.

Mahakama za Kadhi pia tumezipanua. Zimekuwa nyingi makadhi tumewaongeza number yao ni wengi sasa. Tumewaweka wa chini, halafu wa district halafu wa province. Halafu pia tumeweka Chief Kadhi ambaye atachaguliwa ni Waislamu wenyewe.

Tumesema pia kwamba kutakuwa na tume na kutakuwa na ofisi ambayo itasikiliza malalamiko ya wananchi. Pahali ambapo wananchi wanaweza kwenda kushtaki. Kumshtaki polisi, kumshtaki councillor, kumshtaki mbunge, kumshtaki officer wa serikali yoyote ambaye amewadhulumu. Tumeweka ofisi yake sasa.

Halafu tukasema provincial administration haipo tena. Tumependekeza hivyo maanake wananchi walilalamika sana. Kwa hivyo

ofisi kuanzia ya assistant chief, sub-chief mpaka chief, DO, DC, PC hakuna tena.

Pia wale askari, admininstration police tumewaondoa tutawatia kwenye regular police. Police force iwe mmoja tu maanake hawa walikuwa wanaambatana na hii provincial administration. Tumesema pia wale police sasa, police force tumeitoa jina lake tunaita police service. Na polisi wanatakikana kazi yao sasa waifanye kulingana na utumishi wa wananchi. Sio pale zamani ambapo walikuwa wakifanya kulingana na sheria zao za wanavyofikiria ni sawa wananchi walilalamika sana kwamba wanadhulimiwa na polisi, kwamba hawana uhuru wa kufanya wanavyofanya kwa sababu ya polisi, kwamba polisi wakiwashika wanawatesa sana, unaandikiwa charges ambazo hukufanya unashikwa na pombe unaandikiwa bangi na kadhalika. Tumesema sasa kazi zao wao ni watumishi na tumeweka sheria nyingi sana na mwisho ikiwa polisi amekudhulumu unaweza ukamshtaki.

Halafu tumeunda ofisi za wanajeshi. Tumeziweka katika Katiba, Katiba hii ya sasa haina lakini sasa tumeziweka kwenye Katiba sasa. Ofisi ya wanajeshi, wanajeshi ni akina nani, kazi zao ni nini, navy, army, kadhalika air force tumeweka pale na wakuu wao watachaguliwa na nani, watakaa miaka mingapi, wataondolewa vipi ikiwa wamekosea, kazi zao ni nini za hawa majeshi tumeweka katika Katiba.

Halafu upande wa ardhi. Kwanza tumeunda tume ya ardhi, national land commission permanent ambayo itakuwa hapo. Hii inachukua nafasi ya commissioner of lands na hii tume ya ardhi itakuwa na matawi kila district kutakuwa na matawi ya tume ya ardhi.

Halafu ardhi yote sasa ile ambayo ilikuwa ni trustland sasa itakuwa ni ardhi ya wananchi. Inaitwa community land. Wananchi wenyewe ndio ambao wataamua wataangalia vipi ardhi yao, wataimiliki vipi, wataigawanya vipi, wataiuza vipi, wataitumia vipi ni wananchi sio county council tena, itakuwa ardhi ile ni ya wananchi. Sasa wananchi wenyewe watakaa wao wenyewe waamue kama ni kamati au ni kabila au ni kijiji au ni nani ambaye atakuwa na mamlaka ya kuhusu ile ardhi. Pia tumegawanya ardhi katika sehemu tatu. Kuna ardhi hiyo ya wananchi, community land, kuna ardhi ya mtu binafsi, private land, halafu kuna ardhi ya serikali ya umma, public land na zote tumeziweka wazi kabisa, tumezi-define vizuri.

Halafu tofauti nyingine tukasema wageni ambao sio raia wa Kenya hawana ruhusa ya kumiliki ardhi. Hapo nafikiri watu walilalamika na tumesikia, mgeni aweza kumiliki ardhi kwa kukodi tu na maximum ni miaka tisaini na tisa ile lease ya 99 years lakini mtu yoyote ambaye anaweza kuwa na ardhi akasema ni yake ni mtu wa Kenya tu raia wa Kenya.

Halafu tumesema kuwe na sheria sasa katika Katiba za kulinda mazingira yetu, environment miti, misitu, wanyama, ardhi yetu mmomonyoko wa ardhi hili ni swala ambalo Katiba ya zamani halina kabisa. Lakini sasa imekuwa ni lazima ni sheria kwamba tulinde mazingira yetu. Kukatakata miti ovyo, kulima ovyo ovyo mahali ambamo mna mmomonyoko tumeondoa. Ni lazima wananchi sasa wazingatie na serikali lazima ifuate sheria hiyo ya kuzingatia kwamba mazingira yanalindwa. Hizo ndizo baadhi ya zile tofauti ambazo tumeziona, ni kubwa sana baina ya ile Katiba tuliyonayo sasa na hii Katiba wananchi wamependekeza.

Tukiangalia kwa undani zaidi Katiba yetu tulioambiwa tuandike si ndefu sana wala si fupi sana. Wananchi walitaka kwamba isiwe ndogo na isiwe kubwa mno kwa hivyo tumejaribu na tukapata iko na vifungu karibu mia tatu. Vingine ni vifupi, vingine ni virefu.

Halafu Katiba yenyewe inaanza kwa utangulizi kama nilivyosema, halafu inaenda kuangalia umuhimu wa wananchi vile ambavyo tumepata taabu katika kuja na document kama hii, kuandika Katiba tumeweka sheria ambazo zitaifanya wananchi wenyewe wawe ndio ni askari, walinzi wa Katiba na umuhimu wao ni mkubwa sana. Wao ndio wenyewe wa hii Katiba. Wao ndio watekelezaji wa Katiba wao ndio walinzi wa Katiba kwa hivyo wao ndio ambao wanaweza kuirekebisha tena. Hilo tumeliweka katika kifungu cha sheria na tukasema kwamba wananchi wote wako sawa chini ya Katiba hii. Hakuna mtu ambaye ni tofauti, hakuna mtu ambaye yuko above the law vile ambavyo mlisema wananch wote kama ni Rais,kama ni waziri mkuu, kama ni mtu ambaye hajiwezi, kama mtu ambaye amekatika mguu, kama ni mwanafunzi, sote katika mbele ya Katiba hii tuna haki sawa, tuko sawa.

Halafu pili kifungu sura ya pili tumeweza kuiandika Jamuhuri ya Kenya katika map yake, mipaka yake. Kwa sababu wananchi wa Kenya wengine walisema tunashida ya mipaka baina ya Kenya na Somalia, Kenya na Uganda, Kenya na Sudan, hii Kenya haijasemwa katika Katiba mnasama tu hii ni Katiba ya Kenya lakini Kenya yenyewe iko wapi? Sasa katika sura ya pili wale ambao wamefanya geographia tumeona wameandika hata kwa kama utafuata zile coordinates, utaona kwamba ukifuata fuata na kalamu utapata ile map ya Kenya iko vipi na mwisho tutaiweka hasa hapa map ya Kenya ambayo ilikuwa bado yachorwa.

Na tukasema kwamba mji mkuu lazima bado utabaki kuwa Nairobi lakini bunge litaamua kama sehemu zingine za kitaifa kama mahakama zitapelekwa mahali pengine au bunge litapelekwa kwenye mji mweingine, tumeweka open hiyo. Sio kwamba Nairobi itakuwa capital milele. Wananchi wakisema kwamba tubadilishe, sheria iko tayari.

Na tukasema kwamba official language itakuwa ni Kingereza na Kiswahili lakini sasa lugha ya kitaifa ni Kiswahili. Hilo ni neno ambalo wananchi walitaka na tumeliweka.

Halafu tena tukasema kwamba…..

**Interjection:** Na wale ambao wanataka huu mswada waende huko nyumma tutawapatia huko. Halafu neno lingine tumesema tumependekeza sikukuu za kitaifa wananchi wengine walisema kwamba ni nyingi mno, tukasema kwamba sikukuu za kitaifa ziwe ni Madaraka Day ya tarehe moja June, tarehe kumi na mbili December, Jamuhuri Day, halafu wananchi wamependekeza ile siku ambapo Katiba itapitishwa iwe ni siku ya kitaifa, Katiba Day. Tumeondoa Kenyatta Day tumeondoa Moi Day na hizo zingine zote tumezitoa.

Halafu tumeweka sheria na majukumu katika sura ya tatu ambayo wananchi ni lazima wazingatie na serikali. Democrasia

tumesema lazima iweko, tumesema kwamba sheria ni lazima zifuatwe, tumesema kwamba umoja wa kitaifa lazima uweko, tumesema kwamba hakuna kubaguana kwa aina yoyote kwa rangi, kwa dini, kwa kabila, kwa eneo, kwa kila kitu hakuna kubaguana.

Halafu pia tumeeleza majukumu ya wananchi ni nini. Mkikumbuka wananchi wengi walieleza kwamba serikali ifanye hii, serikali ifanye hivi, lakini sasa wewe mwananchi utafanya nini? Kwa hivyo kuna majukumu ambayo ni lazima kila mwananchi naye awe anaweza kuyafuata. Kila mwananchi ni lazima afuate Katiba. Kila mwananchi ni lazima afuate sheria, kila mwananchi ni lazima afuate usawa.

Jambo jingine katika sura ya nne ni uraia. Ni nani raia wa Kenya? Tumeeleza pale lakini tofauti kubwa ni kwamba tumesema raia wa Kenya ambaye anataka anaweza kuwa na uraia mara mbili kwa sababu watu walilalamika wengine wanasema wanamiji yao huko wanataka kuja huku kwa hivyo raia wa Kenya anaweza kuwa na uraia mara mbili lakini tumeweka vikwazo ikiwa atafanya vitendo fulani basi automatically uraia wa Kenya ataukosa.

Halafu bill of rights, haki za kimsingi. Hizo ndizo nimesema zimechukua nafasi kubwa kabisa. Na tukaweka sheria muhimu kwamba serikali inalazimishwa katika Katiba hii kuhakikisha kwamba haki za kimsingi zinafuatwa. Tumezitoa tumezitaja zile haki lakini tumeilazimisha serikali katika sehemu nyingi hapa vifungu vingi vinailazimisha serikali itafanya hivi na hivi, bunge litafanya hivi lakini kuhakikisha kwamba haki hizi zinatekelezwa.

Kwa hivyo tumesema kwamba ni lazima mwananchi wa Kenya apate elimu ya bure na ya lazima. Elimu ni ya bure na ni ya lazima kwa hivyo akina mama mjue kwamba Katiba mpya ikipitishwa, hawa watoto wote ni lazima waende shule.

Tumesema kwamba mwananchi wa Kenya ni lazima apate matibabu, tumesema mwananchi wa Kenya ni lazima apate chakula, maji. Kwa hivyo ni nyingi sana hizo ukiziangalia hapo.

Tumesema kuwe na usawa kulingana na mila na dini baina ya wanaume na wanawake. Wasidharauliwe wanawake, wasiny’anya’aswe.

Tumesema kuna haki ya kuishi na tukaondoa ile death sentence, bado kuna mjadala kwamba mtu asinyogwe kama amefanya makosa afadhali iwe ni kufungwa milele.

Tumesema kuna haki za wazee wale ambao wamepita umri wa miaka zaidi ya hamsini na tano. Wazee walilalamika ya kwamba wakifika miaka hamsini na tano basi huwa maisha yao yanafupishwa. Hasa wale ambao walikuwa wakifanya kazi. Akimaliza miaka mitano baada ya retire huyo amefanya bidii sana. Sasa tumeweka hapa kwamba wananchi wale wazee watalindwa na serikali na sheria na wana haki zao tumezinakili hapo.

Haki za watoto. Mkikumbuka kuna mswada ulipitishwa juzi juzi ya kuhusu sheria za watoto ni lazima wazazi sasa wamewajibika kuangalia masilahi ya watoto wao. Ukizaa mtoto ni lazima umlee, hii sasa ni sheria. Sio kuzaa mtoto halafu ukamwachia mtu mwingine au serikali imlee. Kwanza lazima umlee mtoto yule na tumetoa mambo yao mengi pale. Cha muhimu kabisa ni kwamba ni kwamba lazima wapate masomo ya bure, na tumesema kwamba kama ni kurekebisha basi kiboko kitumike lakini kisitumike vile ambavyo kinatumika hivi sasa, kuwachapa mpaka wakafa wengine.

Halafu tukarudia tukasema kwamba family, jamii ile ya zamani ambayo ndio imetulea iendelee kuwa ni muhimu katika maisha ya wananchi wa Kenya. Badala ya kwamba watu waishi bila ya family.

Halafu pia tumepatia haki watu ambao ni vilema ambao wasiojiweza kwa sababu ya miili yao imeharibika kwa hali moja au nyingine, tunawawekea nafasi zao hata tumekuja na nakala ya huu mswada ya wale vipofu tuko nao pia. Na tumesema kwamba lugha ziwe zinatumika za vipofu ile sign language pia tumesema hizo zikubaliwe mahali popote ziwe zinatumika.

Halafu uhuru wa dini na uhuru wa mtu kutoa maoni yake. Tumeuweka pale mtu anaruhusa ya kuabudu anavyopenda isipokuwa tu asidhuru wale wenzake waliokaribu. Mambo ya kuweka kelele usiku mzima ile tumekataza. Wengine wanakuta wanafanya ibaada lakini kwa wengine huwa ni kelele. Na uhuru wa dini umesema pia si ruhusa mwananchi yoyote ambaye dini yake haikubali kwamba afanye kazi jummamosi aende kazini. Kama ni mtu wa Sabato jummamosi yeye hayuko kazini na usimfute kwa sababu hakuja kazini. Au ni Muislamu Ijummaa anataka kwenda kuswali, sheria sasa iko hapo anaweza kwenda baina ya saa sita na saa nane huyo usimguse.

Halafu tumesema freedom of expression. Kutoa maoni yako unavyopenda. Unaruhusiwa kutoa maoni yako vyovyote. Usitukane, usikejeli mtu lakini unaweza kutoa maoni yako unavyotaka. Halafu kuna haki ya mwananchi kupata habari zinazowekwa na serikali, sasa imekuwa ni lazima. Sio kwamba uende ofisini uambiwe hayo hamtakikani kuyajua hayo. Sasa sheria imesema kuanzia Katiba hii basi mnahaki nyinyi kuja kutaka information yoyote ambayo iko na serikali na ni haki mpatiwe.

Vyama vya siasa, haki ya kisiasa. Tumesema kwamba kura zote ni lazima ziwe za siri, secret ballot hakuna mlolongo kwa kura yoyote ya umma tumesema hakuna mlolongo wala kunyoosha mkono. Kura ni ya siri kwa sababu tumeweka serikali nyingi sana na zote ni za kuchaguana kutoka kwa kijiji, mpaka location, mpaka district, mpaka province, mpaka national. Tukisema kura ni za kunyoosha mikono, na kazi zingine ni lazima ziwe ni za administration ni za nguvu, kutakuwa haifanyiki kazi ile. Maanake utajua fulani alinipigia siwezi kumwadhibu, fulani hakunipigia, atakiona. Kwa hivyo kura ni siri, kura zote tumeweka hivyo.

Halafu upande wa haki za jamii kuhusu mali, ardhi mali inayomilikiwa na wazee na wamama tumesema kwamba sasa kila mtoto,

kila mtu anahaki ya uridhi kutoka kwa familia yake kulingana na mila yake na dini yake na sheria.

Wafanyi kazi tumesema wana haki zao, wana haki za kugoma, wana haki za kufanya maandamano, wana haki ya kupata mishahara sawa na wana haki wa kujiunga na vyama vya wafanyi kazi yaani trade union.

Halafu kuna rights and fair administration. Mwananchi wa Kenya sasa atakuwa na haki ya kutawalwa ambavyo inatakikana na sheria imesema hapa, una haki ya kutofuata amri ambayo unafikiria sio ya sheria. Inaitwa "right not to obey unlawfully instructions". Kama kuna sheria ambayo haifai lakini mtu anakuambia fuata hiyo una haki ya kukataa.

Halafu tumesema haki ya fair trial. Yaani mtu akishikwa kupelekwa mahakamani ana haki ya kusikilizwa kabla hajahukumiwa. Na wale ambao wameshikwa wamepelekwa rummande pia tumewapa haki zao nyingi sana tukiangalia ni kifungu kizima hicho, kurasa mbili. Tumesema wana haki zao kwanza mtu aliyeshikwa ambaye ni rummande ni suspect hawezi kuwekwa sawa sawa na maabusu ambao tayari yameshafungwa.

Halafu si sawa kuwaweka vijana wameshikwa ni suspects uwaweke na wazee katika cell moja. Hiyo tumesema haifai wala kuwachanganya wanawake na wanaume katika cell tumesema hiyo haifai.

Upande wa kura, uchaguzi. Tumesema kwamba wananchi wa Kenya watapiga kura kwa njia ya siri. Tumesema kwamba umri wa kupiga kura ni miaka kumi na nane. Tumesema kwamba kura zitaandikishwa kila siku sio mwaka wa kura pekee yake. Kura zitaandikishwa kila siku, kila mtu akipata kitambulisho yuwaenda ofisi iko, yuwaandikisha kura. Kila akipata kitambulisho yuwaenda basi kuna kura mwaka ujao, mwaka mwingine aliandikisha juzi lakini wewe unataka haki yako ya kupata kitambulisho cha kura, utaandikishwa kila siku.

Tumesema tutaunda ile tume ya uchaguzi upya na wanachama wake watakuwa hawazidi kumi. Hivi sasa ni ishirini na tatu lakini tumewaweka ishirini na mbili, ishirini na tatu. Sasa tumesema wasizidi kumi lakini kila mmoja atoke katika kila mkoa. Na hii tume itakuwa na kazi ya kuandikisha vyama vya kisiasa. Vyama vya kisiasa vyenyewe hatukusema viwe vine au vitano, tumesema kwamba zile sheria tumeviwekea vyenyewe vitakwisha hivyo hivyo maanake tumetoa sheria ngumu sana ya kuandikisha chama cha siasa. Na vyama vya siasa tumevipatia kazi zao za kufanya, sio kungojea kura pekee yake. Tumesema vyama vya siasa ni lazima viwe vinafanya civic education…….

**Com. Mohammed Swazuri:** Halafu tumesema vyama siasa vikifanya uchaguzi, uchaguzi ule lazima usimamiwe na tume ya nje sio katika kile chama kwa sababu kuna maonevu hutokea pale. Kwa hivyo vyama vya kisiasa vikifanya uchaguzi wao kutakuja mtu ambaye hausiki na kile chama aje aangalie uchaguzi iwe free and fair. Naona akina mama wana taabu kidogo.

Upande wa bunge. Ni kama nilivyosema mwanzo tumesema tutakuwa na mabunge mawili na tena kazi za mbunge

tumeziandika. Sio safari hii ambavyo kila mtu anafanya anavyofikiria ni sawa. Tumeandika kazi za wabunge ni nini na tumesema kwamba itakuwa na nyumba mbili, vyumba viwili, chamber mbili. Halafu tumesema kwamba kutakuwa na wabunge wale mia mbili na kumi wanaochaguliwa, kutakuwa na wabunge tisaini wanaoteuliwa na vyama halafu kutakuwa na wabunge wale wa national council ile upper house ambao watakuwa ni mia moja, sabini watatoka kila wilaya. Moja moja kila wilaya. Thelathini watakuwa ni akina mama hawa watakuwa ni wane kutoka kila mkoa na watu watawachagua directly. Kila mtu atachagua watu wale sabini.

Halafu tumesema mtu kuwa mbunge, wale wabunge mia mbili na kumi tumesema ni miaka ishirini na moja, minimum. Lakini wale wabunge ambao watakuwa kwa upper house ni miaka thelathini na tano maanake ile ni ya wazee ile ni kama inaangalia hili bunge la chini. Na wabunge wote umri wao wa mwisho ni miaka sabini, hata Rais pia ni miaka sabini, hata waziri mkuu asizidi miaka sabini. Na tumesema hata Rais asiongoze kwa zaidi ya vipindi viwili. Na tukasema kwamba ikiwa mbunge hafanyi kazi yake iko ruhusa ya kumtoa.

Jambo jingine ambalo tumelieleza kwa upande wa uchaguzi ni kwamba kura zitapigwa kutumia madebe ambayo ni transparent. Ya madebe ambayo ukiangalia unaona limejaa au bado halijajaa sio yale meusi tena ambayo hamjulikani humo ndani mna nini. Halafu kura zote zitahesabiwa kwenye kituo. Pale pale mlipopiga kura zitahesabiwa pale pale katika kituo kile ijulikane mshindi ni nani na wa pili ni nani na wa tatu ni nani aliyeshindwa ni nani.

Halafu pia tukaeleza upande wa executive yaani utawala. Tumesema kwamba pale presidential powers tumeziweka kazi yake iwe ni mkubwa wa taifa, kuangalia mambo ya Katiba, kuwalaki wageni, kutia saini miswada, kuangalia majeshi, hizo ni kazi zake. Mambo ya kwamba awe ni mkubwa wa chuo, mkubwa wa nini yote yameondolewa na tumezitaja kazi zake hapa, makamu wake pia kazi zake tumeziandika na tumesema tunaweza tukamuondoa Rais kama atakuwa anafanya makosa, anaweza kushtakiwa.

Halafu kuna waziri mkuu naye pia. Huyo atachaguliwa na Rais atapendekezwa na Rais lakini atachaguliwa na bunge. Na wale manaibu wa mawaziri na waziri mkuu wawili pia tumewaweka na kazi zao tumeziandika pale. Halafu tumesema kwamba tutakuwa na mawaziri. Tumesema kuwe na wizara zisizidi, wizara ni kumi na tano pekee yake na waziri ni mmoja kwa kila wizara. Waziri mdogo ni mmoja mmoja kwa kila wizara hakuna zaidi ya hapo na kazi zao tumeziandika hapa.

Halafu mahakama ni kama nilivyosema, koti zetu zimekuwa na shida ya either ufisadi mwingi corruption hongo, au zinachukua mda mrefu sana kuamua kesi au ziko mbali sana. Mtu akishikwa hapa anapelekwa mbali sana Kilifi huko. Sasa tumesema mahakama zisambazwe kila mahali, ili wananchi wapate hukumu haraka haraka, na tumesema tume-abolish corruption katika sehemu zote za Kenya sio katika mahakama pekee yake. Tumeandika pale principle moja national principle ni kwamba hongo sasa itakuwa ni hatia. Anayechukua, anayetoa, anayepokea, anayetumia hao wote wamekula hongo. Sasa ni jukumu lenu sasa wananchi kuona ni nani anatoa hongo, ni nani kati ya watu hawa wote na ashtakiwe na aadhibiwe. Kitu muhimu katika

mahakama tumesema kutakuwa na supreme court.

Halafu sura nyingine tumesema devolution of powers. Yaani serikali sasa zimesambazwa. Tumesema tutakuwa na serikali ya kitaifa, halafu tutakuwa na serikali ya jimbo, halafu tutakuwa na serikali ya wilaya na hii ndio ambayo imepewa nguvu zaidi, halafu tutakuwa na serikali ya location, halafu tutakuwa na serikali ya kijiji. Serikali ya kijiji wananchi wamepewa uhuru waamue kama watafanya uchaguzi au watateua wajumbe wao katika kijiji. Hii itakuwa na watu wasiozidi kumi. Serikali ya location katika wale watu kumi watateuliwa wawili wawili waende katika serikali ya location. Na hapo hapo tutakuwa na mkubwa wa location ambaye atachaguliwa na wananchi. Wale wengine watateuliwa kutoka kwa ile village council lakini mkubwa wa location atachaguliwa na wananchi directly, kutakuwa na debe lake maalum yeye la kumchagua.

Halafu tutakuwa na serikali ya wilaya. Wanachama wake watatoka katika serikali hizi za location lakini district governor au administrator mtamchagua directly. Halafu serikali ya mkoa ya jimbo itaundwa na wale wanachama wa kutoka serikali ya wilaya na powers zake tumeziweka pale na wananch watawachagua wale viongozi wa mkoa. Serikali hizi zote zimepewa kazi zao za kufanya. Kutengeza sheria, kutoza kodi, kufanya marekebisho, kuangalia Katiba tumeziandika pale vile. Na upande wa miji, urban governments hizi tumeziweka sawa kuwa na districts.

Upande wa ardhi. Najua hapa tulisema kwamba tuko na shida ya ardhi Coast Province, tuko na shida kubwa ya ardhi. Kwa hivyo tumeandika pale kwamba ardhi itakuwa ni ya wananchi. Wananchi wa Kenya ndio wenye haki ya kumiliki ardhi tumeandika pale. Kama nilivyosema pale mwanzo tukaziandika aina za systems of land management tumeziweka pale, halafu tukasema kwamba katika miaka miwili ijayo kuanzia siku Katiba itakapopitishwa, bunge italazimika kutunga sheria na ifuatwe hiyo sheria ambayo itaangalia umilikaji wa ardhi, ugawanyaji wa ardhi na maswala yake kutoka nyumma. Kuna mikataba ambayo ilifanywa akina Mazurui mikataba ya akina lenana mikataba ya akina nani ili tumesema katika miaka miwili baada ya Katiba hii kuanzishwa ni lazima mambo yake yaangaliwe. Kama kuna watu walichukuliwa ardhi zao kwa maonevu, mambo hayo yaangaliwe, kama kuna watu walipokonywa either basi watalipwa ridhaa ama mikataba ile sheria zile zitaamua kama watarudishiwa ardhi yao au laa.

Halafu tumeangalia ni kama nilivyoeleza environment, mambo ya mazingira. Halafu upande pesa za serikali na umma, tumesema kwamba kodi ni kitu ambacho lazima kiamuliwe ni bunge. Huwezi tu kuamka hivi kama mkuu wa wilaya au mkubwa wa location ukasema Shilingi tano tano kila mtu. Mpaka kodi yoyote lazima ipitishwe na bunge la kitaifa kwa sababu kuna watu ambao huwa wanafanya wanamitindo hiyo ya kutoza kodi.

Halafu tuna mfuko wa kitaifa, consolidated fund ambao tumesema ugawanywe kitaifa. Utagawanywa kwa kila mikoa, utagawanywa kwa kila wilaya, utagawanywa kwa kila district na location.

Makadirio ya pesa tumeweka ofisi mpya ya mtu wa kukadiria pesa, controller of budget na tukasema kama vile wananchi

walivyosema kwamba tungependekeza kwamba makadirio ya pesa, budget haitakuwa ni siri kama vile ambavyo imekuwa miaka yote hii. Kwamba tunangojea tarehe tano au tarehe kumi June. Hii itakuwa imefanyika karibu miezi miwili kabla. Wananchi watahusishwa katika kupitisha budget. Kwa hivyo ikifika siku ya budget sote tuwe tunajua kwamba tukipitisha kitu fulani, tukiongeza bei ya mafuta tutapata pesa fulani mwaka ujao na kadhalika.

Halafu tumeweka pale kazi za banki kuu ya taifa ambazo hazikuwa zimetajwa. Sasa tumeziweka pale kazi yake moja ni kutengeneza sarafu ya Kenya na tumesema kwamba sarafu ya Kenya isiwe na picha ya Rais aliyeko. Safaru ya Kenya itakuwa na picha za kama ni mlima Kenya, kama nini sheria itapitishwa kuhakikisha kwamba haya yanafuatwa, lakini si ruhusa tena kuwa na sarafu ya kiongozi. Maanake tumesema kiongozi atakaa miaka kumi tu. Sasa tukisema tubadilishe kila siku, tutabadilisha sana. Kama mtu ataishi miaka themanini utakuwa umepitia sarafu nane za watu nane tofauti tofauti.

Public service. Tumesema kwamba wale wafanyi kazi wa umma tumewawekea kazi zao pale, tumewawekea tume yao public service commission lakini safari hii tumeieleza vizuri. Halafu tukaja upande wa polisi. Tumesema polisi sasa tumewapatia jina jipya ni Kenya Police Service badala ya Police Force. Kazi zao ni utumishi wa umma pia tumezitaja kwa hivyo sasa wewe una haki baada ya Katiba hii kumwambia polisi, wewe sikiliza sheria kifungu numbari mia mbili sitini na nne kinasema ufanye hivi na hivi, hio si sawa. Una haki maanake kazi zao zimeandikwa sasa sio ili kwamba ni utumishi kwa umma tu halafu haujulikani utumishi ule ni kitu gani. Sasa tumeuandika hapa kabisa na tumeweka Police Commissioner atakuweko na huyu police commissioner ni kama wale viongozi wote wa umma wanapendekezwa na wanatolewa na bunge. Na kufutwa kwao pia ni mpaka bunge si ruhusa sasa kwao usimame pahali useme wewe police commissioner nimekufuta kazi, haiwezekani. Hii ni ofisi ambayo sasa tumeitia katika Katiba.

Halafu pia sasa tumeunda prisons. Sasa tumeibadilisha jina tunaita correctional services, kwenda kurekebisha tabia maanake prisons ni ule ufungo wa watu wameteswa sana. Jina hilo pia lina maoneo.

Halafu sura ya kumi na tano tumekuja kwa upande wa defense forces, army, navy, air force tumewapatia sasa wako katika Katiba sasa. Kazi zao tumeziweka pale tume pia pendekeza kikao cha kitaifa cha security ambacho kitakuwa na Rais, makamu, prime minister na mkuu wa sheria na wakubwa wa majeshi, hao ndio ambao watakuwa wanaangalia usalama wa taifa, tumeweka ofisi za wale commanding officers, zote ziko pale.

Halafu sura ya kumi na sita tukaja upande wa leadership, uongozi na sheria hii inawahusu Rais, makamu wa Rais, prime minister, wabunge na wote members wa district local council na wote wale ambao watakuwa wamechaguliwa kuongoza taifa watakuwa wanafuata sheria hizi tumewawekea hapa.

Halafu tumeunda tume nyingine mpya na tumezikubali zile ambazo ziendelee zile ziko sasa. Kwa mfano tumeunda tume ya humman rights. Commission on humman rights na administration of justice na hiyo ndani yake kutakuwa na ile inaitwa

Ombudsman, public defender. Hii ni ofisi ambayo kama umedhulumiwa na wafanyi kazi wa serikali unaenda unashtaki pale anaitwa anashatakiwa. Tumeunda pia tume ya kuangalia mishahara ya wabunge na wafanyi kazi wa umma, kuna tume yao pia.

Halafu mwisho tunaenda upande wa nani anaweza kubadilisha au kurekebisha Katiba. Tumesema kwamba ikiwa kuna jambo lolote ambalo linataka kubadilishwa katika Katiba hii ijayo lakini linahusiana na citizenship, uraia au bill of rights, haki za wananchi za msingi au serikali aina ya serikali, muundo wa serikali au umoja au uhuru wa wananchi au mipaka ya Kenya, mambo hayo hayabadilishiki mpaka kupitia kwa referendum, kwa wananchi. Hawa wabunge wana haki ya kufanya marekebisho mengine yote, lakini hayo tuliyoyataja haiwezekani mpaka waite wananchi kama hivi, wazungumze nao, wawaeleze wakubali, wapige kura ya maoni ndio kutabadilishwa kwa hivyo hii ni njia tumefanya isiwe ni urahisi watu mia mbili kwenda kukaa halafu kupitisha mara moja, mambo yameshapitishwa. Kwa hivyo kwa sababu wananchi ndio wamehusika sana katika kubadilisha Katiba, ni wao ndio ambao wana haki ya kubadilisha. Kwa hivyo kwa hayo machache sasa nitawapatia nafasi wale ambao wangependa kuchangia katika mjadala huu. Ikiwa kuna mahali ambapo unaona si sawa useme. Ikiwa kuna mahali ambapo unaona tupaondoe au kuna sehemu ambayo ilikuwa mmeisema haipo mseme, lakini mazungumzo zaidi yatakuwa baada ya coordinator na wanachama wake wa kamati kupanga ile mikutano yenu ambapo sasa mtakuwa mnafanya kwa uangalifu zaidi. Asanteni sana. Kama mtu anataka kuongea anyooshe mkono halafu tutasikiliza watu wane, watano kabla hatujajibu. Sema jina lako wakati unauliza swali. Haya wazee Katiba ndio hiyo mwasema je?

**Samuel Shena:** Kwa majina naitwa Samuel Shena. Na kama, pengine labda si swali lakini pengine labda pahali fulani pafafanuliwe zaidi. Nafikiri kama sisi raia wa Kenya tuna uhuru wa kupiga kura. Lakini hata hivyo ikija wakati wa campaign tunawekewa mpaka. Tunaambiwa labda waalimu hawaruhusiwi kuingia katika campaign. Sasa sijui kama jambo hili mmelichukulia vipi? Tunataka kila mtu kwa sababu ana uhuru wa kupiga kura kuwe na uhuru wa kila mtu afanya campaign kuchagua yule anayetaka. Wengine wasiwekewe mipaka. Asante.

**Nixon Nzai:** Kwa majina naitwa Nixon Nzai. Kunayo mambo matatu ambayo ningetaka kuyataja. Jambo la kwanza ni kutoa shukrani sana kwa kazi ile ambayo imefanywa na tume. Naona wamefanya kazi nzuri sana. Sasa jambo ambalo ningetaka kuulizia ama liweze kuwekwa wazi zaidi ni kuhusu huyu prime minister. Katika hii draft tuliyoipata tunakuta kwamba hakuna qualifications ambazo zimewekwa kwa ajili ya huyu prime minister. Naona ingekuwa vizuri kwamba kuwe na qualifications zake ziwekwe, ijulikane ni mtu ambaye anastahili kuwa na kiwango gani pengine cha elimu na kadhalika.

Jambo jingine ni kuhusu hii police services. Mmesema ya kwamba imebadilishwa jina na sasa itakuwa police services. Naonelea ya kwamba hii police services ingefanywa iwe a professional body. Kwa sababu tunaona ya kwamba mara nyingi polisi wamekuwa wakiny'any'asa na kudhulumu watu na hii nafikiri inatokana na vile baadhi yao unakuta kwamba mtu anachukuliwa anakuwa recruited anaenda kwa mda wa miezi sita, hajajua mambo yoyote ya ku-deal with public. Sasa kunakuwa saa ile public relations tunaona kwamba kama ingefanywa kwamba wanaoenda kwa ajili ya kufunzwa mafundisho ya upolisi, wawe ni watu ambao wamehitimu kwa kufikia kiwango fulani, tena isitoshe wanapoenda badala ya miezi sita kwa kile

kikundi cha chini, waweze kuenda kwa mda mrefu zaidi. Na wanapoenda huko wafunzwe masomo yanaoambatana na public relations, sio kwenda tu kufundishwa pengine kushikilia bunduki halafu wakija huku wanaanza kusumbua watu.

Jambo jingine ambalo nataka kuulizia ni kuhusu hii devolution of powers. Mmesema ya kwamba kutakuwa na councils, village councils, locational councils. Katika hiyo draft tumeangalia na kuona kwamba ni nani ambaye atawalipa hawa watu? Kwa hivyo hayo ni mambo ambayo ningetaka yaweze kuelezewa kwa kiwazi. Asante.

**Joseph Mwanyale:** Mimi kwa majina ninaitwa Joseph Mwanyale ninawakilisha chama katika Muhela Location kama chairman. Bwana wa tume nimesikia ukisema kwamba katika vyama vyote vya kisiasa vitakuwa vikipatiwa pesa, vile ambavyo vitakuwa viko bunge. Na pia tulipotoa maoni tulisema kwamba katika sisi tunaowakilisha vyama kama serikali imepita, iko mamlakani na sisi tuko katika mashinani, tuangaliwe kwa sababu sisi tunafanya kazi ambayo ni ya kiserikali, tunatumika lakini malipo hatuna. Kwa hivyo hapo sijui kama tungefafanua zaidi kwa sababu ikiwa ni Kanu imeshinda na sisi tuko katika mashinani, tumeshika tu mkia lakini mara nyingine tunaona kwamba tuna watoto wanasoma tunahitaji pia tuone mambo tuko mbele kama wengine. Asante.

**Daniel Katana:** Kwa jina naitwa Daniel Katana Jefwa. Kuna maswala fulani fulani ambayo ningependa kuyauliza na nipate ufafanuzi. Mwanzo ningeanza kuhusiana na upande wa ardhi. Kuna ile ardhi ambayo imechukuliwa na watu ambao sio wakenya na wamekaa nayo kwa mda tuseme wa miaka tisaini na tisa kufikia sasa, na pengine mda huo umeisha. Lakini sasa kulingana na hii Katiba mpya vile ambavyo wameisikia, ile ardhi wameanza kuiuza na wanaiuza kwa bei ambazo wale raia ama wenyeji waliopokonywa hawawezi kumudu kununua ile ardhi. Kwa hivyo ningeomba Tume ya Katiba ardhi kama zile wasipewe mda mwingine wa ku-lease au kuuzwa mpaka Katiba hii mpya itakapokamilika. Ili ardhi ile kama itawezekana iweze kurudishwa tena kwa wananchi wenyewe iwe trustland na waone jinsi gani watakavyoitumia. Either kwa manufaa ya kujenga mashule ama shughuli zingine za umma. Na pia kuhusiana na hivi vyeo muhimu, kuna kile cheo cha prime minister, cheo cha president, cheo cha deputy prime minister ambavyo ni viwili, vile Kenya inamafundi yasiopungua arobaini na mawili, ningependa kuomba hivi, at no time should the president and the prime minister come from one ethnic group. Na pia hivyo hivyo isiwe pengine president na makamu wake ni watu wanaotoka kwenye jimbo mmoja. Ama deputy prime ministers wote wawili wanatoka katika jimbo mmoja. Mambo kama haya ni mambo ambayo yamenitatiza sana. Utakuta katika serikali ya sasa, kuna sehemu nyingine tuseme hiyo wizara moja basi ni watu wa kutoka pengine sehemu moja ndio ambao wanatawala hiyo wizara nzima. Mambo kama haya yamesumbua sana maongozi ya nchi. Kuna hii sehemu pia kuhusiana na uhuru wa kuabudu. Imewekwa wazi sana lakini kuna sehemu zingine kwa mfano, devil worshiping. Je ni haki raia wa Kenya kumwabudu shetani na kudhuru wengine? Mambo kama haya pia yanastahili kuwekwa wazi kwenye Katiba ili mambo kama haya, watu kama hawa wakipatikana kuwe kuna vifungu fulani vya sheria ambavyo vinaweza kufwatwa na kushtakiwa na kufungwa. Kwa sababu tumeona mambo kama haya yameleta mathara sana hasa kwa mashule.

Na kulingana pia na elimu nchini kuna vitu vingine ambavyo ni muhimu sana kama vyuo vikuu. Tunaona kufikia sasa vyuo vikuu

vimekuwa vingi katika Kenya, lakini tumeona kuna mikoa mingine ambayo pengine tuseme kwa mfano kama Pwani, mkoa wa Pwani ni mkoa ambao tunaweza kusema kwamba unastahili kuwa na chuo kikuu lakini hatuna hata kimoja na vyuo vikuu vimekuwa nje, na vyuo vimekuwa vingi na pengine tume-concentrate mahali fulani. Tungeomba Katiba ijayo ambayo tunaitayarisha at least kila mkoa uwe na chuo kimoja. Hii mikoa minane ambayo kwa sasa inaishi Kenya at least kila mkoa uwe unaweza kuwa na chuo kimoja. Kwa hayo machache, asanteni.

Na pia kingine kidogo kuna kitu kidogo ambacho pengine ningependa kuongezea tafadhali sana. Tunaunga mkono kabisa hii Katiba mpya, tunawasifu, mmefanya kazi nzuri, ni Katiba ambayo inatupendeza na sisi wananchi, sisi raia tunapenda tufanye uchaguzi na Katiba hii mpya kwa sababu ni yetu tunajivunia. Ni Katiba ambayo ni yetu na tunajivunia na tukiwa tutafanya uchaguzi na Katiba ile ya zamani, basi tutakuwa tunafanya uchaguzi na Katiba ambayo haitufai. Na sio Kenya tutakayokuwa tunaipenda, itakuwa ni ile Kenya ambayo hatuipendi. Kwa hivyo serikali iambiwe yakuwa wananchi wanataka uchaguzi ufanywe na Katiba mpya kwa sababu ndio yao, ile ingine hatuijui.

**Emmanuel Charo:** Mimi ningependa kupongeza kazi hii ya tume hii, jina naitwa Emmanuel Charo. Napongeza tume ya Katiba hii ambayo tunazungumzia siku ya leo, nikujua kwamba kweli kama ilivyoandikwa ndio maoni ya mwananchi. Kwanza ningetaka kuzungumza juu ya hudumma ambazo ni muhimu ambazo mwananchi huwa anazihitaji. Na nimesikia ukisema ya kwamba Nairobi itabaki kuwa mji mkuu. Sasa sielewi kama hudumma kama vile driving license itabidi ukitaka uende Nairobi, ukitaka title deed ni lazima uende Nairobi ama hudumma hizo pia zitarudi mikoani. Naona hapo mgekuwa wazi mkatuambia ili hudumma hizo tuzipate hapa karibu.

Kuhusu mipangilio mliopanga, Rais, prime minister, hapo ni sawa kabisa. Na hata nguvu ambazo mlizitoa huku juu mkazitawanya kila mahali, hio ndio maoni ya mwananchi. Twataka hata hawa wabunge wakienda huko bunge, wasitunge tu yao waje watuambie, bali watwae vile vilio vya wananchi na kwenda kuvijadili huko bunge.

Na pia kuhusu jeshi la polisi kama ilivyopangiwa naona ni muhimu. Nguvu zao pia nao zivuliwe. Wasiwe watu wa kuny'any' asa bali wawe watu wa kutoa hudumma.

Kuhusu uraia naona wale ambao ni wageni na wanaenda na milango ya nyumma na kupata uraia, Katiba mpya ikatae kabisa. Kama ni uraia, mtu aweze kufwatwa kule anapotoka ajulikane alifanya nini, isije ikawa anataka uraia tu hapa Kenya ili apate mahali pa kujificha. Lakini kuwe na vithibitisho ambavyo vinaonyesha ya kwamba record yake ni njema, na hata tukimkubali, hataweza kutuny'any'asa.

Nikigusia pia uhuru wa kuabudu, kamba ikilegea sana mambo yataenda mrama. Wale wanaoabudu mashetani, wale ambao wanaabudu mtu binafsi, nafikiri mambo hayo hayawezi kukubalika. Katiba hii iangalie mambo hayo na kuona ya kwamba uhuru huo hauzidi kipimo. Yangu ni hayo.

**David K. Mwaringa:** Jina langu ni David Kamutu Mwaringa. Mimi nikutilia mkazo na kuunga mkono vile wale wenzangu walivyosema. Lakini kitu ambacho kinataka kitiliwe maanani sana ni kwamba, huo uchaguzi ambao uko karibu na kua, ufanywe na Katiba hii yetu. Maanake wakati ule hatukuulizwa kitu sisi. Wakati wa Katiba zile zilizopita hatukuulizwa chochote. Tumeona tu maombo inaenda. Ukishikwa unaenda, ukiachwa unarudi. Ukitaka unaenda, usipotaka unaenda. Sasa wamefikiria wakaona wamefanya makosa. Wamerudi kwetu kuja kuuliza vile tunavyotaka. Sasa haraka hii yote ni ya nini ya uchaguzi, uchaguliwe na Katiba ya zamani? Mambo ya zamani tunataka iishe ndio sababu tumekuja tukaulizwa na tukahitaji haya mapya. Kama inawezekana ama sauti hii yangu itapelekwa kwingine, uchaguzi wa mwaka huu usiwe mpaka Katiba hii ipitishwe. Kwa hayo machache, Mungu ambariki.

**Joseph Karisa:** Mimi kwa jina naitwa Joseph Karisa natoka Bamba. Ninafurahi sana kwa kupata nafasi ya kuja na kusoma hii draft na kuelezwa na Commissioner hii draft. Mimi ningependa kuuliza Commissioner, mmesema kwamba elimu itakuwa ya bure. Toka hapo Katiba ambayo tunataka kuigeuza imesema elimu ni bure lakini sivyo. Sasa mtuambie hii itakuwa bure kuanzia wapi mpaka wapi. Maana unaanza primary unakuta kuna malipo fulani, secondary inazidi, university hasa ndio hatuwezi tukaingia wengine kwa jinsi ya ummaskini. Kwa hivyo mtueleze wazi hii elimu ya bure itaanza kuanzia nursery mpaka university?

La pili mmesema kwamba kutakuwa na village council na pia kutakuwa na district council na provincial council. Je hawa ambao watateuliwa watakuwa na kiwango maalum cha elimu? Na watafanya kazi kwa mda gani?

Jambo jingine ningependa kuuliza ni kuhusu colleges. Sisi watu wa hapa Pwani tumepata taabu sana. Juzi juzi kulikuwa na mambo ya kuandikisha wanajeshi, mambo ya kuandikisha watu kwenda kwa health services lakini wale wote ambao walijaribu kutoka sehemu yetu huku hawakuweza kuenda na pia walikuwa wanafaa kwa hizo qualifications na hadi sasa nasikia wameanza wengine kuenda kwa sehemu nyingine. Je, kutakuwako na mpango maalum kwa kila district kuwa na sehemu fulani ya watu kuchukuliwa kwa kusomea jambo fulani katika wizara fulani? Kwa hayo machache nauliza tume itupatie majibu. Asanteni.

**Joseph Mwangunza:** Mimi nashukuru sana. Mimi kwa jina naitwa Joseph Mwangunza. Jambo la kwanza hapo zamani tulikuwa na kiwanda chetu cha sukari kule Ramisi. Na kiwanda kile vile kilivyopotea ni jambo la kusikitisha sana. Sasa hio ni jambo la kwanza. La pili hata ukiangalia sana sisi waKenya tukitaka kwenda kuchukua vitambulisho, hatuwezi kupata kile kitambulisho mpaka tukatoe Shilingi mia moja ndio tupate ile kitambulisho. Je hii ni haki kwa mKenya kwenda kutoa Shilingi mia moja kupata kitambulisho? Ningependa Commissioner watueleze zaidi juu ya hili ili na sisi tujue tuko wapi.

**Joseph Charo:** Kwa majina naitwa Joseph Charo. Mimi langu ni oni moja tu kuhusu hii siku ya sherehe ya Katiba. Mimi ningependa tuibadilishe iwe ni Ghai Day kwa vile huyu jamaa ametusaidia sana kwa kutungia hii Katiba mpya hasa tumkumbuke yeye na tutakumbuka Katiba yetu. Iwe Ghai Day instead of Katiba Day. Asanteni.

**Kazungu K. Mwabaya:** Kwa jina naitwa Kazungu Kadenge Mwabaya. Mimi nimekuja kuchelewa kidogo basi sijui kama maoni yangu itakuwa……..

**Interjection:** (inaudible)

**Kazungu K. Mwabaya:** Jina langu naitwa Kazungu Kadenge Mwabaya. Nimekuja kuchelewa kidogo sijui kama yale yaliosomwa yanaruhusia mtu kutoa maoni mengine au niyajibu yale ambayo yamesomwa maanake yangu ni maoni. Yote ni sawa. Sasa mimi, tulikuwa tukija hapa mahali kwa mikutano ya sherehe za kitaifa. Nikasikia kwamba yanazungumzwa habari ya magonjwa na ummaskini yatapigwa vita kivipi? Lakini nikaona ya kwamba, kuna jambo ambalo linatatiza kidogo kwa sisi raia ambao hatuna kazi, kwa sababu utakuta wale ma-officer wengi ndio wanaopata riziki lakini sisi raia hatuna chochote tunachopata kutoka kwa serikali. Kwa hivyo maoni yangu ikiwa kwamba, serikali itenge kama billioni tatu kwa kila kipindi cha miaka mitatu ya uchaguzi, ili wananchi nao wapate kunufaika kwa sababu haya magonjwa hayataenda bila matibabu na mtu hataweza kujimudu bila chochote akiwa hana kazi wala elimu naye ni mwanadamu kama sisi. Hayo ndio maoni yangu machache, na Mungu atubariki.

**Samson Mwambire:** Kwa majina yangu naitwa Mwambire Samson. Tumesikia, tunashukuru kwa vile tume ilivyopanga lakini yangu nilikuwa nataka kuulizia ni kuhusu habari hii ya pombe. Pombe kuna beer na pombe zingine lakini kuna pombe moja ambaye ikitumiwa inasemwa ni haramu. Ile hali, ile ya haramu. Ni vipi ambaye amekunywa beer na amekunywa mnazi wote wanaitwa walevi. Jambo hili litafanywa vipi ili tuone kwamba haki na usawa unatendeka? Asanteni.

**Com. Mohammed Swazuri:** Haya, tutaanza kujibu maswali ambayo yameulizwa au kutoa ufafanuzi wa yale mambo ambayo watu wameelezea. Wengine wametoa comments yaani wametoa maoni yao, na wengine wameuliza maswali.

Swala la public servants kuhusika katika upande wa kura. Civil servants kama waalimu kufanya campaign, hilo limo katika zile tunaziita code of ethics za public servants ambao zinawahitaji kwamba, wao wana-serve public service kwa hivyo hawana haki ya kufanya campaign, kusaidia au kuhakikisha kwamba mtu wa chama fulani au aina fulani anapata uongozi. Kwa hivyo bado wale tunawazuia kutokana na ile public code of ethics.

Halafu Bwana Nzai akauliza kuhusu qualilifications za prime minister. Kweli hatukuziandika pale kwa sababu tumesema, prime minister atakuwa ni mbunge kwa hivyo kwanza atachaguliwa mmoja kati ya wabunge. Na tumesema qualifications za wabunge. Lazima awe na at least form four tena form four pass, sio form four tu ile ya D+ au ya E. Form Four lazima iwe ya pass. Sasa akishachaguliwa kuwa mbunge sasa ndio ile chama kilicho na wabunge wengi zaidi ndio Rais atateua mmoja wao awe waziri mkuu. Kwa hivyo indirectly iko hiyo. Huwezi kuwa waziri mkuu mpaka uwe mbunge. Huwezi kuwa mbunge mpaka uwe form four na pass.

Na police service ni kweli tumeeleza hapa. Tumeandika kwamba police service ni lazima watafundishwa mambo ya kuwahudumia wananchi sio kule kushika bunduki tu kama unavyosema. Watakuwa na training ambayo itakuwa ni professional training ya public service na mambo ya public relations.

Bwana Baya amesema kuhusu mambo ya chama. Sisi vile ambavyo tumesema hatukusema kwamba wale wanachama wafuasi wa Kanu au wafanyi kazi wao walipwe. Hiyo hatukusema lakini tumesema tu uchaguzi na uendeshaji wa kazi za vyama sasa utaangaliwa na electoral commission. Kwa hivyo ikiwa kuna maswala yoyote hayo, yako katika sehemu hiyo na vyama vimeambiwa viwe free and fair, vifanye uchaguzi regularly na viangalie wanachama wao inavyotakikana. Lakini kutaja pesa hizo hatukutaja.

Kefwa amesema kwamba kuna zile ardhi ambazo zinamilikiwa na wageni na zile lease zimeisha sasa wanaziuza kwa bei ambayo wale wenyeji hawawezi ku-afford. Hapo tumesema kwamba kama tume unajua hii Katiba tumeipendekeza haijaanza kufanya kazi. Sio kwa upande wa ardhi pekee yake tumesikia vitu vingi vinaenda kwa haraka haraka hivi sasa kwa sababu wanaogopa au kuwania hii Katiba, tumesikia hivyo hatujui ukweli uko wapi. Nyumba zinauzwa, vitu gani vinafanywa hivi haraka haraka ili Katiba ikianza, wawe watu wameshamaliza vitu vyao. Lakini Katiba hii sheria hapa imesema kifungu cha ardhi kwamba, baada ya Katiba hii kupitishwa, tutaipa taifa bunge miaka miwili kuchunguza mali zote na ardhi zote za umma. Itaanza kutumika pale kwa hivyo hata naifanya hivi sasa hiyo bado itaanza kutumika. Ichunguzwe na ikijulikana kwamba ni ya haramu, sheria imesema hapa kwamba itabadilisha. Kwa hivyo hata mtu akiiba nini sasa, aombe Mungu tu hii Katiba mpya isifanye kazi lakini ikifanya kazi, vitapatikana.

Upande wa president na prime minister wasitoke sehemu moja. Tumesema those principles za governors hapa tumezitaja kwamba kunapochaguliwa viongozi wa kitaifa au kwenye chombo cha kitaifa, tume ya kitaifa, shirika la kitaifa tumesema kwamba watazingatia eneo watu wale wapotoka, kila eneo ipate mtu wake, kila dini ipate mtu wake, kila kabila ikiwezekana ipate mtu wake yaani, kila jinsia ipate mtu wake tumesema distribution according to vitu kama hivyo. Kwa hivyo sithani kama itawezekana kama Rais ametoka Coast Province, prime minister pia atoka Coast Province hiyo haiwezekani.

Upande wa devil worshiping watu wengi wamesema kwa kweli hapo ni kweli tunakubali tutaenda kuiangalia. Haiko wazi kwamba devil worshiping imeharamishwa, hiyo tutaenda kuangalia.

Halafu upande wa elimu ukasema kwamba vyuo vikuu ni lazima kuwe na chuo kikuu katika kila mkoa, hiyo ni kweli haipo. Halafu ukasema unataka uchaguzi chini ya Katiba mpya. Uwezo huo uko na watu wengine sio sisi.

Halafu Emmanuel Charo akauliza kama hizi hudumma ambazo tunazifuata Nairobi saa hii. Je zitapatikana hapa? Nafikiri hiyo section imesema wazi kabisa kwa sababu tumesema powers tume-devolve nguvu za serikali tumezitoa pale juu tumezipeleka

mitaani, zimesema wazi kabisa hudumma zote zipatikane pale chini kabisa, zote. Kwa hivyo itakuwa haina haja kufuata driving license Nairobi. Haina haja pia kuifuata Mombasa, sasa utaifuata Kilifi ikiwa tutafuata Katiba inayokuja.

Citizenship upande wa uraia. Tumeweka kitu tunaita citizenship registration board. Hii ni ofisi ambayo itakuwa inaangalia wale wanaotaka registration lakini ni wageni. Kwa hivyo kuna ofisi maalum tumeiweka, kwa hivyo watachunguzwa kabla ya kupata registration wale ambao ni wageni.

Elimu ya bure Bwana Joseph Karisa, elimu ya bure itaanzia pre-primary mpaka standard eight. Hapo ndio tumesema iwe ni ya bure na ya lazima. Halafu tukasema kule secondary school serikali ifanye mipango ya kuirahisisha. Na njia moja tukatoa ni kwamba lazima kutatoka bursary ambazo zitaenda kwa wale kwa kweli hawajiwezi sio watu ambao baba zao wananafasi halafu wanapewa bursary. Tumeandika hiyo kwamba bursary pia zitatoka ziende zitoke kwa serikali zisaidie elimu ya kiwango cha juu nayo pia iwe iko chini zaidi. Kwa hivyo ile ambayo itakuwa bure kabisa ni ya kutoka nursery mpaka primary. Maanake tumesema hivyo ni haki za watoto imetiwa katika haki moja ya watoto. Huwezi kumwacha mtoto asipate haki yake kwa sababu baba yake hana pesa.

Upande wa qualifications za wale village, location na mpaka serikali ya majimbo, hiyo ni kweli haipo tutakwenda kuiangalia na wata-serve miaka mingapi. Nafikiri tulikuwa tumesema kwamba wata-serve hata wao miaka kumi lakini naona tukiangalia imeondolewa haiko kwa hivyo tutaangalia hapo.

Halafu uandikishaji wa wafanyi kazi kama polisi na majeshi ambayo inasemekana kwamba wanakuja hapa lakini wale wetu hawaandikwi. Ajabu ni kwamba tulipokuwa tukizunguka kutafuta maoni, ndio ulikuwa wakati ambapo huo huo nao wanazunguka sijui ilikuwa ni polisi au majeshi. Kwa hivyo kila tukifika mahali tunaambiwa walikuwa hapa jana, kila tukifika mahali, walikuwa hapa juzi. Lakini hii complain tumeisikia Kenya nzima sasa sijui wale wanaochukuliwa wanatoka wapi. Manaake nilipoende Kisii, Wakisii walisema walikuja wakachukua watu lakini sio Wakisii. Nilipoenda kwa Wakikuyu wakasema walikuja hapa jana wakachukua watu lakini hakuna Mkikuyu. Nilipokuja Mombasa nikaambiwa walikuja hapa wakachukua watu lakini hakuna Mijikenda. Mjaluo ni hivyo hivyo. Mpaka Western Province nilipofika wakasema hivyo hivyo. Sasa sijui wale askari huwa wanachukuliwa ni akina nani.

Lakini katika devolution of powers tumesema serikali ya wilaya ndio ambayo itaandika wafanyi kazi wake. Serikali ile ya wilaya ndio itafanya recruitment. Sasa nikipoteza nyinyi wenyewe msije mkasema kwamba tumeandikiwa watu ambao sio wetu. Itakuwa ni yule district governor na council yake ndio ambao mtawalaumu.

Joseph Mwangunza mtambo wa Ramisi. Katika serikali ya majimbo na serikali ya wilaya zimepewa ruhusa kuanzisha kutekeleza mitambo kama hiyo. Sasa itakuwa ni jukumu letu sasa, sio la kule tena. Tukishindwa ni sisi wenyewe.

Na vitambulisho ni bure. Kama mtu yuwakutoza pesa sasa utaenda kwa public defender, Ombudsman ukashtaki lakini ni bure kitambulisho.

Bwana Mwabaya amesema serikali itenge billioni tatu kupewa wale wasio na kazi. Na nilikuwa naitafuta hiyo sehemu, kuna sehemu ambayo imesema kwamba hapa serikali lazima ihudumie wale ambao hawana uwezo lakini sikuipata vizuri. Nitaiangalia halafu nitakujibu.

Pombe ya mnazi. Nafikiri kuna pombe imesemwa ni ya haramu haikutajwa lakini nafikiri ilikuwa ni hii pombe ya mnazi. Hatukuitaja katika Katiba sababu ni nyingi sana tuliambiwa hizo. Wale Wabaluya kule walisema wanataka Busaa ihalalishwe. Wakikuyu wakasema wanataka muratina ihalalishwe, Wataita wakasema wanataka denge ihalalishwe. Yaani hizo ni pombe za kienyeji za kila mahali wananchi wote wamesema wenyewe wanataka wahalalishiwe. Hilo hatujalisema lakini tutaliangalia. Haya maswala mengine, kama yapo. Ni nani mwingine?

**Interjection:** (inaudible)

**Com. Mohammed Swazuri:** Lakini ikiwa wengine wameridhika, ikiwa wamemaliza.

**Yusuf Kassam Haha:** Jina langu naitwa Yusuf Kassam. Baba yangu alizaliwa India na mama yangu ni Mkenya. Shida ambayo tunayopata sasa ni vitambulisho na uraia wa Kenya. Sijui Katiba ya sasa inatuangalia vipi ndio swali langu?

**Interjection:** (inaudible)

**Yusuf Kassam Haha:** Alizaliwa India wa kutoka India na mama yangu ni Mkenya. Sasa sijui Katiba mpya yatuangalia vipi sasa? Asante.

**David Chanzera:** Mimi kwa majina naitwa David Chanzera. Ningetaka kuzungumzia hii sehemu ya amendment ya hii constitution. Ni vizuri hii constitution hii draft tumetengeneza sisi wananchi, lakini tukiangalia hata ile Katiba ya kwanza ilipotengenezwa na vile iko sasa, sio ile iliotengenezwa kule kwa sababu ya hizi amendments. Hawa wabunge wamepatiwa nguvu na hata pengine kupitia kwa vishawishi waka-amend hii Katiba. Je hatuoni kwamba kuna hatari ya kwamba hawa hawa wabunge ambao sasa wengine wanakataa kuna uwezo watoe hizi bills na zipitishwe, wabadilishe vifungo ambavyo sisi tunaonelea vinatufaa kwetu? Kwa hivyo nataka uelezee kama kuna sehemu ambao nyinyi mmewafunga wabunge ili wasiibadilishe hivi hivi vile wanavyofanya ile Katiba ya zamani. Asanteni.

**Amos Kazungu:** Kwa majina ni Amos Kazungu Keya. Mimi ni chairma wa shule. Msione kwamba nitakuwa nafanya pigo kidogo. Maoni yangu mimi ni kwamba kuna haya mambo ambayo tumesema kuanzia nursery mpaka darasa la nane litakuwa

halina malipo. Lakini sasa tunaona kwamba kuanzia darasa la kwanza mpaka la nane huwa waalimu wanalipwa na serikali lakini sasa kuna hawa waalimu wa malezi ambao ni waalimu wa nursery. Tunawalipa sisi wazazi. Sasa itakuwaje ikiwa itakuwa ni bure hawa watalipwa na nani? Kwa hivyo ninaomba kwamba ikiwa inawezekana, hao waalimu wa nursery walipwe na serikali ili watoto wasome kwa wingi. Asante.

**Elias Jefwa:** Kwa jina naitwa Elias Safari Jefwa natoka Sokoke. Ninaomba nafasi hii kuzungumzia kidogo swala ambalo linanitatiza kimafikira kuhusu Katiba ilikuwa ikiendelea na ile ambayo iko kwa sasa. Kama hii idara ya Electoral Commission itatusaidia vipi na hili swala kwa sababu naona ndilo limeadhiri sana kati ya hawa wananchi wote ambao hasa kama hatujaangalia nilikuwako kama mwalimu wa Katiba na nikaona kwamba matatizo kama tunataka kuchagua viongozi ni wale ambao kidogo wana ufahamu wa mashule kwa sababu, hawajalitia maanani sana wale viongozi wa kule mashinani pia hawana ile ufahamu wa uongozi ambapo watatuletea shida kama tutapata viongozi kama hao ambao kidogo wameadhirika kimasomo, itakuwa haitatusaidia kwa sababu bado kutakuwa kule mashinani kuna giza na hatuwezi kuanza kilele kule. Kama ni diwani, awe pia ataangaliwa na hiyo Electoral Commission na ahakikishiwe kwamba huyu kweli kimasomo anaweza kulea ile jamii ambayo iko kule ndani.

Na pia sehemu nyingine ambayo iko hapo, hata kama Electoral Commission imetuahidi kwamba tutakuwa na huo uhuru wa kupata hivi vyombo kutoka huku kwa section ndogo kabisa sio ati tutegemee kutoka national lakini hata kwa ma-district pia tutakuwa tunapata hivi vyeti vya kuwa pengine kama driving license, kama haki za mashamba yetu. Pia ituhakikishie kwamba, kwa mda ambao tumengojea hizi hati zetu kama za mashamba, zinatoka mapema inavyowezekana kwa sababu sasa tumekuwa na hofu kwa sababu tumekuwa tukiahidiwa kila wakati kwamba itatoka na hiyo kwa hakika haijatoka na hatuna tena hofu yakuwa itatoka. Kwa hivyo naona ingehakikishiwa kwamba itatiliwa mkazo zaidi kutoka kule kwa Electoral Commission kwa sababu wale viongozi tuko nao huku mashinani hawafwatilizi ule mshururu wa sheria na wanaweka wananchi kuwa waoga kwa sababu ya vitisho vya hizi ofisi za administration. Ukifanya kitu kidogo kwa sababu mtu haujui haki yako, inasemekana wewe utaenda kufungwa kwa hivyo tafadhali kutoe mafunzo fulani ya kuwa mtu anajua akipitia na hapa yuko sawa kwa sababu tuondoe ile hofu ya wananchi kutafuta zile haki zao. Asanteni.

**Morris Sifa Kahindi:** Jina langu naitwa Moris Sifa Kahindi. Ningependa kuzungumzia mambo manne. Jambo la kwanza ni kama vile officer hapa commissioner ameeleza kuhusu swala la mnazi. Kama vile ametuelezea umesema ya kwamba jambo hili bado hamjaliweka katika Katiba. Na kwa maoni yangu ninafikiri mgejadili kuhusu jambo hili kwa sababu kutojadili kwenu kuhusu hili jambo la mnazi, naona limefaidi sana hawa askari ambao wanafanya kazi katika hizi sehemu zetu. Winners huwa ni hawa askari kwa sababu wanatumia hio nafasi kuny'any'asa wananchi na kuwahangaisha huku na huku. Kwa hivyo nafikiri ingekuwa vizuri kama ingejulikana mnazi ni halali, ijulikane ni halali kama si halali, ijulikane si halali. Badala ya kuwapa askari nafasi ya kuitisha pesa kwa akina mama na wachuuzi wote wa mnazi nafikiri hilo si jambo ambalo linafaa kabisa. Kwa hivyo ningependa sana tume ifikirie sana kuhusu jambo hilo.

Pili, ningependa kuunga mkono msemaji mmoja ambaye amezungumza kuhusu Katiba ile ya zamani na ile ya sasa katika upande wa ubadilisho. Nafikiri tungetaka hii tume ama tungetaka uhakikisho, baada ya mambo mazuri na maoni mazuri ambayo yametolewa na tume ikayapokea, tunashukuru. Lakini je, tutahakikishiwa vipi kuwa hii Katiba mpya haitabadilishwa kama vile ilibadilishwa ile ya kwanza? Kwa sababu hiyo ya kwanza pia ilikuwa nzuri sana lakini baadaye ikapitia mikoni mingine ambayo hatuelewi. Je, hii mpya ambayo tunaiona ni nzuri leo tutakuwa na uhakika gani kuwa nayo haitarudi kama hii ya zamani vile ilibadilishwa? Jina naitwa Moris Kahindi.

Tatu, tunajua hii tume yenu inapigwa vita. Hii Tume ya Marekebisho ya Katiba tunajua inapigwa vita kwa sababu kuna wale ambao hawapendi ama hawaridhishwi na yale maoni mazuri ambayo wananchi wametoa. Kwa hivyo basi hata ingawaje tuna moyo na tuna hamu ya kufanya uchaguzi kwa hii Katiba mpya, lakini hata hivyo hivyo tuna hamu, wananchi wana hamu na moyo wa kuondoa wale viongozi ambao wamekuwa hawatuongozi vizuri kwa haraka iwezekanavyo. Kwa hivyo nilikuwa nataka kukuuliza hivi, je hii tume yenu how soon ama mtamaliza hii kazi kwa mda gani mfupi ujao ili tupate ile nafasi ya kuondoa wale viongozi ambao tumewakataa?

Jambo la mwisho nafikiri kuna msemaji amegusia kidogo lakini ningetaka tu nizungumze kuhusu hawa askari. Nafikiri kama officer alivyosema ni kwamba hudumma za serikali hazifai kununuliwa. Tumetajiwa vitambulisho mambo ni mengi sana lakini kuna hudumma moja ambayo pia ni kama ambaye tunanunua wa kila siku kupitia kwa hawa askari wetu. Saa hii ukienda uki-report kuwa kuna kitendo fulani ama umefanyiwa kitendo fulani, askari lazima umnunue ndio aende hapo mahali. Mara nyingine ukienda uki-report police unaambiwa gari ya polisi haina mafuta lazima ujaze petroli ndio gari iondoke iende hapo mahali. Je hii ni haki kweli kununua huduma kama zile? Ni hayo tu asanteni.

**Benson Baya Mwanyale:** Mimi kwa majina naitwa Benson Baya Mwanyale. Niko na mambo mawili. La kwanza in kuhusu hawa akina mama maanake wako na maneno lakini naona wanakaa hivyo tu kwa hivyo ninawakilishia.

**Interjection:** Wanasemaje?

**Benson Baya Mwanyale:** Hawa akina mama mimi naona narudi nyumma kutoka baada hatujapata uhuru tulisema tunafukuza wakoloni ili kulikuwa kuna watu ambao wananunua watu huko nyumma. Sasa tukilinganisha na hawa akina mama siku hizi, iko hii mambo ya mahari hii ambayo imeenea sana. Sasa imekuwa ni kama utumwa. Unakuta mama unaenda kwao huko umempenda, ukifika huko baba yake anasema lete elfu hamsini, lete elfu thelathini, unaona. Halafu unakuja kukaa naye hapo miaka miwili, mitatu, mine, mitano mmepata watoto kama wawili, watatu, wane hivi mara mmekorofishana. Mara unasema lete hao watoto, wewe nenda kwenu huko, umenipotezea wakati kabisa. Sasa unakuta yule mama anaenda nyumba wakati amepoteza, ametoa watoto na watoto naye ndiye aliyewachunga amewaweka kwa tumbo lake miezi tisa, bwana alikuwa anaangalia tu anatoa ile mishale yake halafu yeye anaangalia tu. Sasa wao akina mama, naona sisi wababa tunawany'any'asa sana. Sasa akina mama nataka wapate haki yao pia. Ikiwa ni watoto, muwe mtafanya share. Ikiwa ni watoto sita naye

umpatie angalao watatu na yeye ajifarijie. Hiyo ni maoni yangu. Hiyo ni maoni ya akina mama nawakilishia maanake nimeona kitambo wanakaa tu.

Mambo yangu ya pili ni hivi. Kuna huu ugonjwa wa ukimwi. Msikize akina baba na akina mama. Tuna ugonjwa wa ukimwi ambao unamaliza watu hata hivi dakika hii watu wanakufa. Na sisi tunasikia tuna serikali sijui serikali ni mimi au ni yule sijui, ni sote. Sasa basi swali langu ni hivi, sisi tunaisha na ukimwi na kama umeshikwa na ukimwi inasemekana unaweza kupata angalau miaka miwili, mitatu ukajisukumma maisha yako. Lakini sasa basi ukienda kwa hii habari ya hospitali zetu hizi pengine mwili wako haujioni vizuri, vile bado unaongea yeye mtu tayari amekuandikia sijui madawa mangapi tayari hata hajui amekupima uko vipi. Yeye ameandika tayari nenda ukachukua hizo nini huku uende zako. Halafu mimi huko nyumbani naenda kukaa na nakesha na huo ugonjwa, nikimrudia asubuhi ananiamba hizo madawa zote nilikupatia jana wewe hujatosheka nazo? Basi mimi siwezi tena.

**Interjection:** (inaudible)

**Benson Baya Mwanyale:** Sijui kama atakuwa amenipa zipi?

**Interjection:** Kwa upande wa ukimwi unasema aje?

**Benson Baya Mwanyale:** Kwa upande wa ukimwi tunataka tusaidie hawa watu ambao wana ukimwi. Tuwasaidie kama ni madawa, kama kwa njia yoyote ili wapate nao eh ni hivyo tayari.

**Com. Mohammed Swazuri:** Akina mama sijui huyu Bwana Baya alivyosema ndio hivyo ama mwasemaje? Hakuna neno kama hilo? Mimi nimeuliza akina mama, nimeuliza akina mama sikuuliza nyinyi wazee. Wana midomo yao wale nao. Haya. Tujibu haya maswali ya mwisho. Bwana Yusuf Kassim ameuliza habari ya uraia. Kulingana na kifungu nambari kumi na saba cha Katiba hii mpya, wewe ni raia wa Kenya. Pia baba yako au mama yako ni mKenya, basi wewe ni raia wa Kenya kulingana na kifungu nambari kumi na saba.

Halafu wabunge. Tutafanyaje kama wanataka, tutawazuiaje wasiwe wakibadilisha Katiba kiholela? Nafikiri kitu ambacho tumechukua hapa, tumechukua ile tumeiga ile sheria iliyokiweko katika Katiba ile ya Lancaster ya mwaka sitini na tatu. Ile Katiba ilikuwa haiwezekani kubadilishwa na wabunge ovyo ovyo ndio tumeileta hapa. Inasema, ikiwa kuna mswada wa kubadilisha Katiba, kwanza itataka bunge la chini two thirds majority kuanzisha ule mswada. Halafu pia liungwe mkono na two thirds, theluthi mbili ya upper house. Na unajua hiyo sio kazi rahisi. Mara nyingi huwa hawaelewani, si kazi rahisi. Halafu pia ukishamaliza zile katika ule mswada una stages, first reading, second reading, third reading. Saa hizi ni urahisi sana ni majority simple majority katika stage nyingine, lakini tunaweka katika kila stage ni lazima iende na hiyo hiyo two thirds majority. Kwa hivyo hapo tukakuta itakuwa ni vigumu sana kwa hao kurekebisha Katiba kiholela. Lakini nimeeleza pale mwanzo kwamba kwa maswala fulani ambayo tumeyataja si kazi yao kabisa kwanza, ni ya wananchi kama hii tena. Kwa hivyo hio imeleta

jukumu kubwa sana kwetu sisi kuilinda Katiba yetu na sisi tuna haki sasa kwa Katiba hii kusema kwamba mapendekezo ya marekebisho yaliyofanywa ni haramu. Wananchi wakisema hivi inakuwa ni hivyo, mna haki ya kufanya hivyo. Nimesema kwamba haitakuwa sawa kwa mwananchi wa Kenya kukubali sheria ambazo zenyewe ni unlawful. Una haki ya kuzikataa.

Halafu nani atawalipa--

Viongozi lazima wawe na kiwango fulani cha elimu, hilo tumekubali kwamba hatukuliweka kwa wale viongozi wa zile serikali za chini kutoka kwa jimbo mpaka kwa village, hiyo ni sawa, tutakwenda kuweka.

Na haki za mashamba. Hili swala la mashamba haki zake ni kama swala la mahakama. Tulisema kwamba matatizo ni kwamba katika mahakama kesi zinachukua mda mrefu. Na katika swala la mashamba pia ni hivyo hivyo. Kuna title deeds ambazo zimekaa miaka kumi, watu wanafukuzana nazo hazipatikani. Tumesema hapa tutatengeneza sheria katika miaka miwili ijayo kuhakikisha kwamba maswala ya kupata haki yanafanyika haraka. Halafu pia kuna kesi za mashamba. Kuna watu ambao wana kesi za mashamba, wale wazee waliokosana na shamba hilo walikufa, lakini watoto wamerithi hizo kesi na mpaka leo hazijaisha au ni uongo?

**Audience:** Ni kweli.

**Com. Mohammed Swazuri:** Na hizo families zitaelekea hivyo mpaka sijui lini. Kila ukifika kesi yapelekwa hivi, yapelekwa hivi. Sasa tumesema pia tupitishe sheria kwamba kesi yoyote ya mashamba au ya nini mwisho wake uwe ni miaka miwili. Kesi zote ni lazima ziamuliwe katika miaka miwili. Ikizidi hapo sasa hiyo kuna mambo mengine hapo. Kwa hivyo tumesema mambo ya title deeds na mambo ya kesi za mashamba kwanza zitasikilizwa na wazee ndio tuende juu halafu ni lazima zimalizike haraka katika miaka miwili.

Halafu ukasema kuhusu civic education. Wananchi wengi walipendekeza kwamba kuanzia sasa iwe ni lazima kwamba wananchi wafundishwe. Wengine walisema ianzie shule, wengine wakasema kwenye mihadhara na kadhalika. Sisi tumeitaja katika sehemu zote hii na tumeipatia viongozi, tumeipatia sana hawa vyama vya siasa. Ukiangalia hapa katika kazi yao moja muhimu kubwa kabisa, vyama vya kisiasa ni civic education kuhusu mambo haya ya Katiba.

Pombe ya mnazi mmetaka tukayajadili kwa sababu hapa ndio panapatikana faida kutokana na wale polisi. Hilo tutakwenda kulitia mkazo.

Halafu ukaeleza Bwana Kahindi kuhusu urekebishaji wa Katiba na bunge, nimeshajibu hilo. Halafu unataka kujua tutamaliza kazi yetu haraka inavyowezekana vipi ili tuweze kuenda kwa uchaguzi. Tumesema kwamba tukimaliza hii stage hii kuna ile stage ya kongamano la taifa. Mkutano wa kitaifa wa Katiba ambao tumeupanga uwe tarehe ishirini na nane mwezi huu. Na

wale delegates pia wameshachaguliwa. Si wale wawakilishi wako hapa wale watatu? Yuko mmoja hapa, ameshachaguliwa. Kutakuwa na watu mia sita na hamsini au zaidi ambao wataangalia haya maswala ambayo mnayauliza nyinyi. Wao watakwenda kuyaangalia neno baada ya neno na sheria imesema wakae kule Nairobi, watakuwa Bomas of Kenya kwa mwezi mmoja mpaka waafikiane. Sasa wakishamaliza pale kutakuwa ni November ishirini na nane. Halafu tena italetwa yale marekebisho yatakayozungumzwa pale yataletwa kwetu ili sisi tuyarekebishe, tena tuandike tena, halafu na sisi tupeleke bunge. Kwa hivyo sisi kulingana na sheria tuliyopewa, kazi yetu itamalizika tarehe tatu mwezi wa January. Hiyo ndio programme yetu. Tungependa sana ikiwezekana tupate mda ili hizi structures tulizosema, haya mabadiliko tuliyoyasema yawe yatakuwa yanatekelezwa. Lakini sasa wananchi wanasema wanataka uchaguzi. Kuna wananchi waliosema wanataka uchaguzi mwaka huu kwa vyovyote vile. Hatutaki kama ulivyosema, tunataka wale viongozi ambao ni wabaya tuwaondoe haraka inavyowezekana. Halafu sisi tumesema kwamba tutamaliza January. Sasa hivyo vitu viwili kidogo vimekosana hapo. Mwisho wetu sisi ni January na mwisho wa wanavyosema wenyewe ni kwamba uchaguzi wataufanya mwisho wa mwaka huu. Sasa uamuzi si wa tume tena, uamuzi ni wa viongozi na wananchi. Sisi tu watumwa ndio maana ya tume hiyo, sisi tu watumwa. Tukitumwa kwamba tufanye ili Katiba imalizike, tutafanya. Tukitumwa kwamba nendeni mkafanye tutawapatia miezi miwili, mitatu mhakikishe kwamba hizo serikali nyingine mmetengeneza, ofisi zao mmetengeneza, tutafanya. Kwa hivyo uwezo sio wetu sisi tena, tutaepuka kando kidogo tuwaachie nyinyi na viongozi wenu, wabunge. Hao ndio wana haki ya kueleza itakuwaje. Ingawaje hata sisi tungependelea kwa maoni yetu kwa vile tumetengeneza Katiba haina haja tena iwekwe kando. Sisi wenyewe maoni yetu ni kwamba, tutengeneze Katiba ili itumike katika huu uchaguzi unaokuja.

Halafu swala la mwisho lilikuwa ni yule Bwana aliyesema anatoa maoni ya akina mama halafu akasema hayo ni maoni yangu kuhusu upande wa mahari. Kwamba mapendekezo yake ni kwamba watoto wagawanywe baina ya mama na baba ikiwa watakuwa wamekosana. Nafikiri hii tumeitaja indirect lakini tumesema itategemea mila, desturi na dini. Hatuwezi kuingilia ya kwamba tuseme watoto mkikosana basi tutawafanya hivi. Mila nyingine watoto ni upande wa kwa mama. Mila nyingine watoto in upande wa kwa baba. Dini nyingine ni hivyo hivyo. Sasa hapo hatuwezi kuwafunga watu.

Halafu akazungumzia habari ya ukimwi, nafikiri serikali inaangalia swala hili. Kuna dawa ambazo zinasemekana ni za bei ya rahisi ambazo zitasambazwa kwa wale ambao ni wagonjwa. Nafikiri hayo ndio maswala ambayo tumeyachukua. Nafikiri tutaishia hapo, nyama ikiwa tamu ukiitafuna sana hutoka ladha, tutawaachia ambao wanataka kuchangia zaidi kwa mikutano ambayo Bwana Mwaringa na kamati yake watawapangia ambayo itakuwa ni ya ndani zaidi ili kutueleza vile ambavyo mnafikiria tufanye. Yale mliyosema tumeyasikia na mtaona matokeo yake. Lazima tutakwenda kubadilisha tena mpaka wananchi waseme kwamba ndio kweli, sasa hii ni document ambayo kila mtu imemridhisha.

**Interjection:** (inaudible)

**Com. Mohammed Swazuri:** Haya, wa kwanza ni wewe.

**Mohammed Sharrif Omar:** Katika hii Katiba, jina naitwa Mohammed Sharrif Omar. Katika hii Katiba tumegusia maswala ya ardhi. Katiba hii, nafikiri kuna ardhi ambazo mpaka dakika hii ziko kotini haswa tukitizama zile ardhi ambazo ni crown land, serikali zimechukua zikagawanyia watu, siko kotini mpaka leo. Lakini sisi tukasema itakuwa rahisi katika Katiba hii, inaweza kupitishwa hii maswala ya ardhi yakatatiziwa mara moja kulingana na mapenzi ya raia wenyewe. Crown land ni ardhi za watawala. Ni ardhi ambazo zilichukuliwa na watawala wa zamani waliokuwa wakitawala hapa. Sasa katika hii Katiba nafikiri wakati ule hapa nilichangishia mimi. Nilikuwa tu ninaomba hii Katiba kwa sababu Katiba ndio uamuzi wa kipekee, mara ni wa raia na raia ndio serikali. Kenya hivi sasa ni huru kwa hivyo mali yote ambayo ilikuwako ni ya watawala inarudi kwa Mwafrika huru. Kwa hivyo napenda hizi crown land katika hii Katiba, Katiba ikipitishwa crown land zote zirudishwe kwa serikali na wagawiwe raia wale wanakaa katika hizo ardhi.

Pili tumegusia kuhusu civic leaders, civic education hio itakuwa muhimu sana ikiwa itakuwa ni somo la kilazima ifunzwe shule ili kila mtoto akinukia anajua ni kazi gani mfanyekazi wa serikali anapaswa kufanya. Kila wizara atakuwa anajua ili kusudu asipate kudanganyika.

Halafu ni kuhusu viongozi. Unajua sisi wakati mwingine hua tunafanya makosa. Tunaweza kumpigia kura mtu tukadhani ni mzuri, tukauzwa kwa pesa kidogo, tukauzwa miaka mitano halafu mtu yule akaja badilika na mapozi na maringo na kutuny'any' asa. Kwa hivyo napenda Katiba hii sisi tuwe tuna uwezo. Tukimwona mtu anatumia mamlaka yake vibaya, tuweze kumtoa mara moja, vote of no confidence, tunaita DO, DC kwa kazi zote tunasema huyo hatumtaki ndio tunapenda ipitishwe.

Niligusia siku moja hapa kuhusu mambo haya, magonjwa ya zinaa, uasherati ambao umeenea huku kwetu, sehemu yote nchi nzima. Magonjwa haya ambayo yanatupata saa hii. Haya magonjwa serikali na organization mbali mbali wanatafuta mbinu za kukomesha ugonjwa ama kupunguza. Nikatoa maoni hapa, tukasema, kuna hawa watu hapa, lesbians hawa na Malaya wanaochangishia zaidi katika huu ugonjwa. Kazi zao ambazo wanatoa huru kuzifanya katika mabaa na miji mikubwa mikubwa utakwenda ona watu wanatembea uchi wanawake. Mimi nasikitika siku moja nilikuja kusikia katika vyombo vya habari wakisema, Mombasa Pwani kuna malaya wengi, na ni kweli. Lakini tukiangalia malaya hawa ambao wako huku, huku si makwao. Wengi akienda kwao havai vile anavaa huku. Mimi siku moja niliuliza mwanamke moja, nikamuuliza, hivi unavyovaa auntie halafu hata nyumbani unavaa hivi? Akasema, sasa huko nyumbani nikifika kwa stage tayari huwa navaa vizuri najua naenda kwa baba kwa mama, lakini huku sina relative, sina mjomba, sina nani kwa hivyo mimi sina wasi wasi. Kwa hivyo sisi tulikuwa tunaomba hao watu wachukuliwe hatua. Serikali katika hii Katiba, ipange Katiba ipitishwe, wale wanawake wanaovaa nguo fupi wasiruhusiwe kuvaa nguo fupi hadharani. Kwa sababu hata wanaharibu pia hawa vijana wanaoinukia. Ukiona amevaa nguo uchi kabisa juu hapa wasiruhusiwe na wakipatikana wachukuliwe hatua. Washikwe na kufungiwa kifungu cha sheria washtakiwe. Halafu pili wasipatiwe ruhusa ya kufanya kazi ya ummalaya kwa mabaa. Afadhali hio ni confidential wakifanya shauri yao kama vile bangi imepigwa marufuku lakini inaendelea kuuzwa mpaka sasa lakini kisiri, kiheshima basi wao pia wafanyi hivyo hivyo lakini uhuru hatutaki. Asante.

**Kiboni Kiraga:** Mimi kwa majina naitwa Kiboni Kiraga na nilikuwa nataka nichangie katika hii Katiba yetu kuhusu mambo ya shule. Nafikiri kuna wenzangu wameongea juu ya chuo kikuu karibu kiwe kila mkoa, lakini hawakuongea kuhusu national schools. Kwa hivyo kwa maoni yangu ningependa katika Katiba hio iwekwe kwamba karibu kila mkoa uweze kuwa na shule za kitaifa. Shule ambazo ziko ziboreshwe ili tuondoe hili tatizo la wanafunzi kupata shule za huko juu na wazazi hawana uwezo na inawabidi watoto wasiende kuchukua nafasi zao huko. Kwa hivyo katika Pwani utakuta hakuna shule yote ya kitaifa. Tungependa hizi ambazo huku zichaguliwe nyingine ziweze kuboreshwa. Kwa hivyo katika Katiba mpya tungependa iwe kitu kama hivyo. Asanteni.

**Samson Kahaso:** Mimi kwa jina naitwa Samson Kahaso kutoka Pala Kumi. Mimi nina maoni ama ninatoa mawazo yangu kuhusu Katiba hii. Maoni yangu ni kwamba Katiba ile ya zamani ambayo kwamba ilikuwa inatuongoza mpaka sasa imetuny'any'asa zaidi sana. Hata ninaomba hii tume ya Katiba ikiwezekana, tuweze kupewa mda mzuri wa kuweza kuwa hatuwezi kuchagua, uchaguzi unaokuja tuchague na Katiba hii mpya ambayo tunatoa maoni wakati. Kwa sababu kwa mfano tumeny'any'aswa kama hivi. Kama vile ambavyo tunatarajia wakati ujao tufanye uchaguzi, unapata wale wenye madaraka makubwa kama Raisi, anaanza kubandikia wananchi mtu tayari anasema huyu ni mzuri badala ya sisi tupewe uhuru tujue Raisi ni nani. Wakati huu tayari tumeambiwa mtu fulani anafaa kabla ya sisi hatujajua tutampigia nani. Mamlaka kama yale hatuyataki ndio tunataka tupewe uhuru vizuri. Ikiwa sisi wananchi tuna haki, tuachiwe haki yetu tuchague yule ambaye tunamtaka. Sio yeye ni Raisi ama ni nani aseme fulani anafaa na sisi hatujamjua yeye yuko vipi. Kwa hivyo ninaomba na kuwaunga mkono wale wenzangu kwamba hii Katiba mpya, tufanye uchaguzi ujao na hii Katiba mpya badala ya kuambiwa fulani anafaa, hatutaki.

**Donald K. Chengo:** Kwa majina naitwa Donald Karisa Chengo. Ningetaka kuuliza swali ama pengine mapendekezo kwa Commissioner wetu. Jambo ambalo ningetaka kuuliza ni kwamba kuna hali ambayo ilikuwa ikiendelea sana na hivi inaendelea na pengine mimi nashangaa kwamba tunaambiwa tuko Kenya huru. Lakini mimi nafikiri hatujakuwa huru bado. Ningetaka kuuliza kuhusu mambo ya public institution. Nikiuliza mambo ya public institutions nitaanza na primary schools, secondary, health facilities zote katika Kenya hii. Kuna uny'any'asaji ambao umewahi kuendelea na unaendelea ambao sasa ningetaka pengine tupate uhakikisho….

**Interjection:** (inaudible)

**Donald K. Chengo:** Uny'any'asaji ni corruption. Corruption imekuwa ikiendelea sana na ningetaka nipate uhakikisho ili sasa mwananchi wa kawaida kama mimi ikiwa nitapata jambo kama hilo niweze kulifwatiliza na nijue nitaanzia wapi. Kuna pesa za shule ambazo zilikuwa zinaliwa sana na hata sasa ninavyosema zinaliwa. Pesa za shule, pesa za public institutions hizo zinaliwa. Na zinaliwa na watu ambao pengine wamepata uongozi mahali fulani na wanachukua jukumu hilo la kula pesa kama hizi. Sasa kitu tunachojua ni kwamba serikali iko na wahasibu wao ambao wamewaandika. Sasa utakuta kwamba sisi kama wazazi ama kama mwananchi wa kawaida akitaka kufwatiliza jambo kama hilo ili ajue pesa zile zitarudi, inakuwa vigumu na inakuwa vigumu kwa sababu hasibu kama yule, kuna fee ambayo ni alipwe ndio aje afanye uhasibu huo katika shule hii.

**Com. Mohammed Swazuri:** Kwa hivyo ulikuwa unapendekeza nini?

**Donald K. Chengo:** Sasa kupendekeza kwangu ni kwamba ikiwa itawezekana, tume kama hili ama tume hii iweze kufanya mpango huo wa uhasibu wa public institutions uwe ni bure ili sasa mambo kama haya yakiwa yamefanyika yaweze kugunduliwa mara moja na mwananchi aweze kulindwa. Asante.

**Timothy Kalume:** Kwa majina naitwa Timothy Kalume. Nina mambo kama matatu hivi. Kwanza kabisa ni kushukuru tume kwa juhudi zote ambazo walizifanya kuhusu hali ya kurekebisha hii Katiba ambayo sasa tunaitazamia.

Pili, nikuomba tume hii izidi kutilia mkazo kuhusu mashirika ya kiserekali na mashirika yasiyo ya serikali ili yaweze kutoa hudumma kwa kamati za maendeleo vijijini.

Halafu tatu, nimesikia kuhusu mpango wa budget hapa. Ningeomba tume hii iweze kuitia mkazo katika hali ya kupanga hii budget ili kwamba kamati hii za maendeleo vijijini ziweze kupangiwa ili kwamba ziweze kutekeleza miradi ya maendeleo mikubwa mikubwa. Asante.

**Emmanuel N. Charo:** Kwa jina Emmanuel Charo. Mimi ningeona ya kwamba huu mda kwa kukodi ardhi miaka tisaini na tisa ni mingi zaidi. Ipunguzwe ili wale waliokodi hata kutoka enzi za uhuru mpaka sasa, hizo ardhi ziweze kurudi kwa wenyewe. Kwa hivyo miaka kama arobaini na tano ama hamsini.

Lingine ni kwamba kuhusu hii pombe ya mnazi. Nafikiri ukiuliza wengi hapa watasema sio haramu kwa sababu haitengenezwi bali hugemwa huo ndio utofauti wake. Zile nyingine utaona wanatengeza, wanachanganya sijui muratina sijui nini, mimi sijui huwa wanasaga wanaweka chinazi, lakini hii nikutolewa pale juu, ikifika saa tisa ya jioni unakuta wazee wanachangamka. Kwa hivyo ni ile serikali mpya ifanye utafiti pia kujenga hata viwanda na pia kutafuta masoko kwa nchi jirani ili hata tuone tutapata mapato.

Jambo lingine nikuhusu hao watoto wa mitaani. Katika serikali ijayo, hao machokora watafutiwe ardhi ambayo wataipewa, itasimawa ni serikali ili waweze kulima na wafundishwe huko ili wao nao waweze kuwa raia bora na pia waweze kujitegemea.

Kuna mwingine nimesikia akisema baba ni Muitaliani lakini akaoa hapa Kenya. Mimi ningesema ya kwamba itakubalika yeye kupata uraia ikiwa yule ambaye aliyeolewa hapa Kenya alitoka katika zile kabila arobaini na mbili. Katika Katiba hii mpya elimu ya jeshini ingeenda kwa ma-primary schools. Ikawa mtu akimaliza darasa la nane a know-how ya mambo ya jeshini. Wengi wetu hapa hata ukimpa bunduki hajui atafanya nini lakini nchi zingine utapata hata mtoto mdogo anajua hayo mambo yanaendelea vipi. Kwa hivyo hiyo elimu iwe ikiingia katika ma-primary schools.

Na swali la mwisho ni hili. Je sisi raia kisheria, twaweza kususia uchaguzi ikiwa tutalazimishwa kufanya uchaguzi na Katiba ya zamani? Asante.

**Nicholas Ndago:** Kwa majina naitwa Nicholas Ndago. Mimi nina swali moja ambalo linahusiana na ajali ambazo hatuzitarajii lakini huwa zinakuwa. Kwa mfano mtoto wangu au mtoto wa raia yoyote hapa apate ajali. Utakuta kwamba ajali kama hiyo inatakikana ulipwe lakini ukitaka kulipwa ni upate wakili ndio kesi hiyo ipelekwe kotini. Ikiwa hauna wakili na ni mtu raia ambaye hauna pesa, kesi hiyo inaenda hivi hivi. Kwa hivyo mtu kama mimi ambaye siwezi kupeana pesa kwa yule wakili, nianzie wapi?

**Japhet Nzaro:** Majina yangu ni Japhet Nzaro. Ninamaswala kama manne hivi ya kuchangia. Kwanza ningependa hawa watumishi wa serikali ambao wanataka kupigania huu ubunge wawe wanatuambia vile wako nyumbani, kwa Kizungu tuseme wa-declare wealth. Kwa sababu kama hawatafanya hivyo mtu anaweza enda bunge mwaka mmoja baada ya miaka mine yaani unamuona pengine amejenga majumba kama hamsini. Hizo pesa atakuwa amezipata wapi? Tunatakikana pengine ameenda pale kufanya mambo zake za kuiba iba ndio akapata hizi pesa akafanya hizo mambo zake. Tunataka tuzijui kwanza zile uko nazo kabla hajachaguliwa.

Halafu kuna hawa ambao kuandikwa na hizi kazi hizi za kura kama sisi vijana ambao wakati wa kura tunaandikisha hizi kura. Tunataka pia tupewe nafasi tupige kura kwa sababu hii Katiba ambayo iko sasa haitupi nafasi kupiga kura.

Halafu kuhusu mnazi. Wale wenzetu wako na hizi cash crops ambazo zimehalalishwa kama kahawa, kama chai lakini hapa kwetu Pwani tukiangalia mnazi ambao ni ule wetu ambao tuko nao ambao tunaweza kujitegemea nao hauandikishwi kama cash crop. Tunatakikana yaani tuonewe hurumma pia na sisi. Tukipewa huo mnazi ili watu wawe wakichangia changia tunaweza inuka pia tukiuuza huu mnazi. Hawa polisi pia nao wawe hawatuingilii vizuri kwa sababu hio Katiba haisemi kama ni halali ama si halali. Mara unaambiwa unaweza ruhusiwa hivi kwa sababu ni wakati wa kura, mara tuachiwe lakini tunataka tuwe kuna mwelekezo sahihi, na vile tunaomba ni tuachiliwe huu mnazi uwe halali.

Halafu ya mwisho ni kuhusu hii hali ya kugawanya hii rasilmali za hapa nchini. Tukiangalia kama huku kwetu kuna vitu ambavyo vinaharibika sana, kama hizi barabara, mambo ya elimu, tunaona tunawekwa kiwango cha chini kwa sababu ukiangalia wenzetu wana barabara za lami kila kitu lakini huku kwetu hakuna. Tunataka Katiba ambayo itatufanya sisi nasi tuwe kama wenzetu. Asanteni.

**Joseph Kenga:** Mimi jina langu ni Joseph Kenga. Kwanza ninatoa shukrani sana kwa tume hii, ile mipangilio vile ilivyo pangika. Lakini langu ni kuomba hasa hii serikali ya majimbo itiliwe mkazo sana. Na sababu ni kwamba tumeona wazi kabisa sisi watu wa Pwani hapa tumeny'any'aswa ya kutosha. Jambo la kwanza ni hiyo mambo ya mnazi inasemekana huku kwetu ni

tembo ya haramu lakini kwao hakuna kitu cha rahamu watu wa bara. Pili ukiangalie hivi utaona hata zile shule ambazo kwamba watoto huwa wanafunzwa mambo ya udereva wa ndege hapa Pwani hakuna mpaka mtoto awe ni mtoto wa mkubwa tena anaenda huko bara. Ukiangalia hivi hata hawa watu wanaotaka kujifunza kuwa madaktari, waganga ambao kwamba wataweza kututibu. Ukiwa unataka upate certificate nzuri ni uende huko Kenyatta National Hospital lakini hapa huwezi kupata hiyo. Sasa tuko Kenya huru, kwa nini kuwe vile vilivyo kule sivyo vilivyo hapa? Hawa wengine nafikiri ni ujamaa ule wa sisi watu wa Pwani hapa kudanganywa. Kwa hivyo mimi ninaomba hii Katiba itilie mkazo kabisa hii serikali ya majimbo. Tuwe na vyetu kama ni kuwa maskini tuwe ni maskini ya Pwani yetu, ikiwa si ummaskini tutajiangalia wenyewe na Pwani yetu. Asante sana.

**Francis Mwangi:** Majina yangu naitwa Francis Mwangi na mambo ambayo ningependa kuyaongea siku ya leo ni mawili pekee yake. Jambo la kwanza nitaongea kuhusu arthi. Jambo la pili nitaongea jambo kuhusu kuabudu. Kuhusu ardhi, tunajua ya kwamba kuna wamazurui walio ingia hapa katika mkoa huu wetu wa Pwani miaka mingi ambao imepita. Na walipoingia katika mkoa huu, hawa wamazurui hawakuja na udongo. Hawakuja na mchanga kutoka kwao uarabuni bali walikuja kitupu. Wakaja wakachukua maili kumi kutoka uvuo wa bahari. Kwa hivyo ile eneo ambalo liko na dhahabu ya Pwani, wakaja wakachukua hawa wamazurui. Walipochukua hio ardhi, serikali ya mkoloni ilipomaliza kazi yake, serikali sasa iliyochukua mamlaka ikampatia nafasi ya kuendelea na kutawala hilo eneo letu sisi wa Pwani. Sasa swali langu ni hili. Saa hii Katiba ambayo tunatengeneza kwa wakati huu inasema ya kwamba baada ya hiyo Katiba kukamilika kuna hatua ambayo itachukulia hawa ambao wamechukua hiyo ardhi yetu. Sasa swali langu ni hili, babu zetu waliny'any'aswa na hawa wamazurui, mashamba yao yakachukuliwa, wakafukuzwa kando. Sisi ambao ni watoto wa hawa wazee katika hii Katiba mpya tutafaidika na nini? Maana yake huyo mtu amenyonya mali yetu kwa huo mda wote. Tutafaidika na nini? Babu yangu amekufa akiwa maskini kwa sababu shamba lake limeshachukuliwa. Sisi nasi tunaelekea kuingia kaburini maskini kwa sababu mashamba yetu vile vile yameshachukuliwa. Sasa tutakufa maskini namna gani na hali mali yetu imechukuliwa? Sasa kwa hiyo Katiba nilikuwa ninaonelea ya kwamba tuangaliliwe kitu chochote na hawa ambao wanaitwa mazurui hata tuweze kupata chochote nasi. Hiyo ni jambo la kwamza.

Jambo la pili ni kuhusu mambo ya kuabudu. Tukiangalia nchi yetu ya Kenya tuko na uhuru wa kuabudu lakini kuna shida moja hapa. Tumepigana na mambo ya kikabila ya kwamba hakuna mtu ambaye anaongea ya kwamba kabila hili ilitokea hapa Pwani iende sehemu pengine za Kisumu na kule kwingine. Sasa watu wote wa Kenya tunaishi kwa njia ya hali ya amani lakini ninaona ya kwamba amani ambayo tunaishi nayo inakuja kuharibiwa ama kunakuja kutokea vita ambayo inaitwa vita vya kidini. Maanake hapa we have Christians na pia tuko na Mwislamu. Mwislamu akiweka mhadhara pale Kilifi mimi nami niweke mhadhara wangu, nikianza kuhubiri Mwislamu ataanza kunipiga mawe. Ataanza kunipura mawe akisema ya kwamba ule Mungu ambaye unaabudu sio Mungu wa kisawasawa. Jambo hili nilikuwa ninataka liweze kuangaliliwa sana maanake tunaweza kuwa tutaacha hii hali ya kikabila lakini kuingie vita vya kikabila katika upande wa dini. Kwa hivyo hio mambo ndio ninataka ya kwamba Katiba hii ambayo tunayochangia kwa wakati huu iweze kuangaliliwa sana katika upande huo. Tusije tukaumia zaidi ya vile ambayo tumeumi. Sina mengi ni hayo tu na Mungu awabariki.

**Nixon Nzai:** Kwa majina Nixon Nzai. Nashukuru sana kwa nafasi hii ya pili. Nataka kuulizia ama kueleza jambo hasa kuhusu hizi kazi za Rais. Tumeonelea kwenye hiyo draft ya kwamba Rais ana mamlaka ama amepewa nafasi yake, Prime Minister pia amepewa nafasi yake. Lakini tunaona kwamba huyu Rais ni kana kwamba yeye ni mtu ambaye atakuwa amechaguliwa na watu wote kwa sababu ameenda kwa kupiga kura kutafuta kama Rais wa nchi. Hivyo amechaguliwa na watu lakini Prime Minister itakuwa ni mtu ambaye anachaguliwa kule bunge na anachaguliwa na kile chama ambacho kitakuwa kimeshinda. Sasa mahali ambapo pameleta utata ni huyu ambaye amechaguliwa na watu na huyu ambaye anachaguliwa na bunge. Pengine ingekuwa kwamba huyu Prime Minister angechaguliwa na watu na huyo Rais awe atachaguliwa na huyo Prime Minister. Naona hapo pengine tungekuwa na …*(sentence incomplete)*

**Interjection:** (inaudible)

**Nixon Nzai:** Kitu kama hio. Halafu jambo jingine ambayo ninataka kuliongelea kuhusu huyu Rais tena ni kuhusu, katika Katiba ambayo tuko nayo hiyo ambayo iko operational saa hizi, tunaona kwamba miswaada mingi ambayo imekuwa ikipitishwa bunge huwa inakawia sana. Yaani unakuta kwamba jambo limezungumzwa limefikia mahali ambapo bado sign ni ya President lakini inachukua mda. Kunako hata sheria ambazo zimepitishwa za union charter lakini unakuta kwamba inapofika mahali pa kwamba ziwe zitakuwa domesticated, hiyo inakuwa kazi ngumu hapa Kenya. Kwa hivyo katika huyu Rais ambaye tutakuwa naye, nafikiri kungekuwa kuna mechanisms ambazo zingemfanya kwamba kunapokuwa kuna sheria ambazo zimepitishwa katika bunge, mswaada ambao umepitishwa katika bunge, kuwe kutakuwa na urahisi wa kuweza kuweka hiyo sign yake badala ya kuwa ameachiwa nafasi ya kuweza kuangalia mpaka mahali pale ambapo ataona kwamba inafaa. Naona kama ni jambo ambalo limepitishwa katika bunge hivyo, inaonekana kwamba ni jambao ambalo limekubalika. Kwa hivyo kungekuwa na direct ama kungekuwa kuna hali fulani ya kumwezesha kwamba aweze kuweka sahihi badala ya kuweka hilo swala likae kwa mda wa miezi hata wakati mwingine wakati wa mwaka mzima kabla jambo hilo halijapitishwa. Kwa hivyo maoni yangu ni kwamba huyu Rais aweze kupewa ama kushurutishwa ili kwamba aweze kuweka sahihi jambo ambalo litakuwa limepitishwa na bunge. Asante.

**Com. Mohammed Swazuri:** Haya mzee nikimaliza utaanza wewe. Swala la ardhi. Tumesema kwamba tumezigawanya ardhi mara tatu. Kuna ardhi ya public lands, kuna ardhi ya private land na ardhi ya community land. Kwa hivyo ile ardhi ambayo ulikuwa unasema crown land, hiyo tumesema itabakia town land lakini trust land ndio tumesema itakuja irudi iwe ya wananchi. Kwa sababu bado serikali inataka kuwa na ardhi ambayo ni lazima iwe inatumia kwa mambo ya wananchi.

Halafu mapendekezo ya kwamba civic tufundishe shule, hiyo tutachukua. Na habari ya kwamba mbunge kama hafai atolewe, tayari iko hiyo.

Halafu upande wa magonjwa ya zinaa kupitia kwa lesbians na malaya, hizi nyingine ni sheria ambazo tayari ziko, watu hawazifuati tu lakini ni sheria ambazo ziko tayari na tulikuwa tumependekeza lakini nafikiri mwisho ilishindwa kuhusu mavazi.

Watu wavae vizuri lakini ikasemekana ile freedom of expression na nini itakuwa sasa umempatia upande huu halafu unatoa upande ule kwa hivyo hiyo kidogo imeleta utata hapa.

Halafu mapendekezo ya kwamba tuwe na national schools, hiyo ni sawa na university kila mkoa. Halafu nguvu za Rais nafikiri tumeshazisema hizo kwamba tumezipunguza nguvu za Rais. Sio kwaba tumeziondoa, tumezipunguza na tumezigawanya kwa watu wengine.

Halafu public funds kuibiwa kwa mali ya umma na kwamba lazima kuwe na audit. Nimesema pale mwanzo kwamba tumepitisha principle katika sheria hii yetu kwamba, uchukuaji, utumiaji, upeaji wa hongo ni haramu. Kwa hivyo na wizi pia wa wale public officers, pia ni sehemu moja ya hivyo. Kwa hivyo kama kuna mali ya umma ambao inaibiwa na wafanyikazi wa serikali, hapa tumeshaondoa hio kwamba ni haramu na mfanyekazi yeyote anayepatikana na mambo hayo ni lazima ashtakiwe. Tena tumesema safari hii kushtakiwa kwake akipatikana na hatia ni arudishe ile mali.

Halafu pendekezo kwamba NGO's na government organs ziwe more responsible, hiyo ni sawa. Na kamati za vijiji kwamba zipangiwe mipango yao ya kifedha, tumesema hiyo tayari iko. Narudia kwamba tumesema serikali inawajibika kugawanya pesa kwa hivyo viwango vyote hivyo. Na siku ile serikali za mitaa zote pia zinatakikana kutoza kodi na kupata revenue ambayo pia wanatakikana kuitumia hapo hapo chini.

Halafu pombe ya mnazi nafikiri nimesema tumeelewa na tutakwenda kurekebisha. Na kuna nchi ambazo tunajua kwamba pombe ya mnazi imekuwa ni industry. Wanatengeneza kwa mtambo haswa na zinakuwa exported, tunazijua nchi hizi.

Lease wamesema miaka tisaini na tisa ni mingi, tumekuwa tumewaka arobaini lakini watu wakasema kuna wale wakulima ambao ni commercial farmers. Wanatusaidia sana, ukiwapatia miaka mingi zaidi wanaweza wakafanya kazi nzuri kuliko kuwapatia miaka michache ndio maana ikarudishwa tisaini na tisa lakini tulikuwa tumeweka arobaini ndio mwisho.

Halafu vijana wale wa mitaani, street children wapewe ardhi yao. Kwanza tumesema tunataka kuondoa hii tatizo ya street children. Kwa nini kwanza hata tuwe nao hao watoto wa mitaani? Si wanatoka kwetu? Ndio tukasema kwamba neno family liweko pale. Wengine wanawatoa watoto mitaani kwa sababu wamezaliwa nje ya ndoa wanafikiria kwamba wale watoto wale hawatarithi ukiwaleta nyumbani ndio wanawatupa. Tumeweka sheria sasa mtoto atakayezaliwa yeyote ni lazima atarithi kwa hivyo sasa watoto tutakuwa tunawapeleka mitaani sisi wenyewe lakini kuna haki ambazo watoto wako nazo, ni lazima tutawawekea. Ingawaje tumesema hapa kila mtoto, haikusema mtoto wa street, mtoto wa nyumbani, tumesema ni kila mtoto. Kwa hivyo ni jukumu sasa la serikali kuangalia maslahi ya hawa watoto.

Halafu mmoja akaeleza kwamba kuna jeshi education ifundishwe, mambo ya majeshi yafundishwe kutoka shule. Hiyo ni sawa lakini naona kuna hatari. Ikiwa watoto watafundishwa bunduki, wako primary school na secondary school na nyinyi mnawajua

vile ambavyo wako siku hizi. Hiyo italeta hatari. Mnaona vile sasa wanachoma mashule na kufanya nini, jambo ndogo kukosa mkate tu wanachoma shule mnafikiria mkiwapa bunduki itakuwaje?

Mtu mmoja akauliza kama tunaweza ku-boycott, kususia uchaguzi unaokuja. Nimesema tume haimo katika mjadala huo maanake sisi bado tu watumwa.

Japhet Nzaro ukauliza kama inawezekana kwa viongozi ku-declare wealth. Iko tumeiweka hiyo. Kuanzia permanent secretary, ministers, wakubwa wa mashirika, MP's, Prime Minister na Rais kwanza ni lazima uta-declare wealth. Utasema mali zako uko nazo ni ngapi na ulizipata namna gani. Hiyo tuko nayo hapa kwenye schedule hapa.

Pendekezo la kwamba wale wanaofanya kazi ya tume ya uchaguzi wawe wanaruhusiwa kupiga kura, hilo tutaangalia.

Mzee moja Joseph Kenga ameeleza habari ya majimbo lakini tumeshasema kwamba yako hapa ni vile ambavyo sisi wenyewe tutayaangalia.

Ardhi za Mazurui tumesema kwamba ardhi zote zilizochukuliwa na wageni katika sheria itapitishwa ya kuhakikisha kwamba zinachunguzwa, na nimesema ikiwa itapatikana kwamba yaweza kurudishwa, itarudishwa. Ikiwa itapatikana kwamba yule aliyetumia kwa miaka mia tatu atoe rithaa, atalipa tumeandika hiyo.

Halafu uhuru wa kuabudu. Tumesema kwamba tumetoa uhuru wa kuabudu lakini tukasisitiza kwamba uhuru ule usiwe unadhuru dini nyingine. Hiyo tumeandika wazi kabisa. Itakuwa si sawa kupiga mwenzako mawe kwa sababu amesema kitu fulani. Tumesema dini zote kila mtu awe na uhuru wa kuabudu, uhuru wa kuhubiri dini yake vile ambavyo inaruhusiwa katika dini yake.

Waziri Mkuu na Rais kwamba Waziri Mkuu angekuwa ndie anachaguliwa na wananchi halafu amchague Rais. Tumesema sisi tunataka Rais achaguliwe na wananchi huyu ndie atateuwa Waziri Mkuu na ndie bunge litapitisha Waziri Mkuu. Kwa vyovyote tunayofanya mmojawapo lazima achaguliwe ni wananchi, mwingine achaguliwe na bunge. Hakuna nchi ambayo tunaijua ambayo wale wote wawili wanachaguliwa na wananchi, itakuwa wanashindana sasa, hatujui mkubwa ni nani. Lakini lazima mmoja awe chini ya mwingine ndio maana huyu atateuliwa na Rais halafu atapitishwa ni bunge na kazi zake tumeshaziweka.

Halafu umesema kwamba sheria ikipitishwa, saa nyingine Rais anakaa miezi mitatu, miaka sita hajatia sign. Sasa tumefunga hio tumesema lazima atie sign katika wiki mbili. Mswaada wowote ukipelekwa kwa Rais kama umeshapitia hizo sehemu zote mpaka bunge, mpaka upper house ikapitishwa sasa ni yeye atie kidole, tumesema maximum ni wiki mbili, hiyo imewekwa. Kwa hivyo hakuna ile ku-dilly dally mara hii mara hakuna hii. Nafikiri maswala mengine ni haya. Mzee wangu ulikuwa unaanza kusema, haya.

**Erastus Hare:** Mimi ninashukuru sana kwa kupata nafasi hii. Serikali ninayopenda mimi kibinafsi ambayo nataka itawale…….Erastus Hare Ruwa nakaa Sokoke. Mimi nataka kama vile ninavyotaka mimi ni serikali iwe ya majimbo. Yaani kila jimbo lisimamie lenyewe halafu wakikata yale mashauri pale kwao, pale katika lile jimbo lao ndio wanapeleka katika Nairobi kule itakuwa ndio serikali kuu ili iangaliwe kwamba walitaka namna gani kule katika lile jimbo lao. Hivyo ndivyo napendekeza.

**Daniel K. Jefa:** Kwa jina naitwa Daniel Jefa, mimi ni mwalimu na ningependa kuchangia swala la elimu. Nikikumbuka ile Katiba ya kwanza ya Lancaster mwaka elfu moja, mia tisa sitini, na mwaka elfu moja, mia tisa sitini na mbili, mambo ya elimu ya msingi yalikuwa yako mikononi mwa mkoa na pia mambo ya elimu ya secondary pia yalikuwa yako mikononi mwa mkoa. Kufikia hivi sasa ukiangalia Kenya, waalimu wamekuwa ni wengi, watoto wamekuwa ni wengi na imekuwa ni vigumu hii serikali kumudu hiyo sector ya waalimu, ndipo kufikia hivi sasa, tuna mgomo wa waalimu. Lakini kama majukumu haya yangesambazwa katika mkoa na wilaya watu wakasimamia wenyewe elimu ya msingi, wakawa na madaraka kabisa ya kupanga juu ya elimu yao ya msingi, aina ya syllabus vile itakavyokuwa na curriculum mpaka kiwango cha secondary halafu serikali kuu ikasimamia elimu ya chuo kikuu.

Tukiangalia nchi kama Canada na America ina mfumo aina hii na wanaweza kusimamia elimu na inaendelea vizuri sana. Kwa hivyo kama hili swala lingeangaliwa hivyo kila mkoa ungejimudu, ungejitahidi na ukapata kushindana na mikoa mingine na hata kiwango cha elimu pia hapa mkoani kwetu ingeenda juu. Na pengine zile mikoa mingine ambazo hazijiwezi kielimu, ile serikali kuu ingeweza kufidia kimapato ili nayo ihakikishe ya kwamba kwa mfano Eastern Province tuseme pengine haitakuwa na rasilmali zake haiwezi kumudu kusimamia mpango kama huu. Ile serikali kuu ipate kusimamia mpango kama huu ili ndugu zetu kama wale nao wasiachwe nyumma. Kwa hivyo wananchi wakiwa watawajibika wenyewe kuangalia elimu yao ya msingi na ya secondary school, basi kutakuwa kuna hali nzuri sana kwa sababu hakuna jimbo ambalo litakubali kuachwa nyumma kwa sababu elimu ndio rasilmali kubwa kabisa.

Utakuta kulingana na Katiba ya sasa, hii rasilmali ya elimu haijawahi sawa sawa. Kuna sehemu nyingine zinaendelea zaidi, zimenufaika zaidi, zimepata misaada mingi zaidi upande wa elimu lakini kuna sehemu nyingine zimeendelea kubaki nyumma. Kwa mfano kumekuwa na swala la national schools, kumekuwa na swala la vyuo vikuu. Kwa hivyo sector kama hii kama ingeletwa kwa wananchi wenyewe wakajipangia. Kwa mfano mkoa wa Pwani, tunamaadili yetu ambayo tuko nayo, mila na desturi zetu. Hizi pia tungependa kuona katika ile syllabus ama curriculum inayofundishwa mambo kama haya yameingizwa ndani. Kwa hivyo haya maswala haya ndio nilikuwa nataka nichangie. Asanteni.

**Joseph Baya:** Mimi kwa majina naitwa Joseph Baya. Nawashukuru kwa sababu umetangulia bwana officer ambaye unahusika kwamba majimbo iko tayari. Lakini mimi ningechangia kwamba, ningeomba kwamba kusiwe hali ya ukabila lakini mapato ya kila mkoa iwe inaweza kuendeleza ile sehemu. Kama kwa mfano kama port tuko nayo, mapato kama serikali kuu

huko Nairobi pengine iende kama kumi na tano namna hii lakini ile nyingi ibaki hapa. Na pia ningeomba kwa mfano kama Pwani yetu utalii ndio umejaa sana lakini tunakuta kwamba chuo kiko kule. Tungeomba kwamba sehemu ile ambayo inahusika kama ni kahawa, factory ziwe huko huko. Kama ni utalii ni Pwani, iwekwe namna hiyo. Pengine ningeomba kwamba hata kama mabaraza ya miji, yale mapato yote isiende yote kule barabara ziko mbaya. Ingeweza kuwekwa pale ili mshahara madiwani wakapata na mabarabara nayo ikafanyika ili hudumma wananchi wawe wanapata kwa sababu kama ni ushuru unatoka hapo, halafu inaenda kule tunangoja mishahara kutoka kule.

Ingine ni kwamba factory pale ambapo zinaanzishwa kama ni jimbo la Pwani, tuone kwamba ni watu elfu moja wanaajiriwa, mia saba na hamsini wawe wanakaa pale pale. Si tuletewe watu kutoka jimbo fulani, na ikiwa ni jimbo fulani amekuja kwa sababu hatuna kiwango hicho cha elimu lakini kuwe kuna 15% inabaki pale ili tuone na sisi tunachapa chapa hapa. Asante sana kwa hayo machache.

**Kazungu K. Mwabaya:** Jina langu ni Kazungu Kadenge Mwabaya. Nashukuru sana kwa kupata hii nafasi ya pili ili kutoa maoni. Maoni yangu ni kuhusu sehemu kame ambazo hazina baraka ya mvua kila wakati. Unapata kwa wakati mwingi kuna jua kali sana na watu wanateseka kwa kiu ya maji pamoja na wanyama. Kwa hivyo tunaomba katika sehemu hizi tuweze kupatiwa vifaa tukaweze kupata mahali ambapo tutapata maji kwa urahisi maanake shida hiyo utakuta, mtoto wa chini wa miaka kumi na sita anawekwa mtungi wa lita ishirini ababe zaidi ya kilomita tano. Hata yeye mwenyewe kama ni asubuhi, ni vigumu kuenda shule. Na sehemu ya pili katika huo, ukulima wake nao umekuwa katika hali ya shida. Kuwe kuna angalao michango tukaweze kupata yale majembe ya kukokotwa ili tukaweze kuendelea zaidi.

Kuongezea zaidi ni katika sehemu ya utawala. Maanake katika sehemu ya utawala kusema au kutunga inakuwa ni rahisi. Lakini kutenda inakuwa ni vigumu. Kwa hivyo katika ule ugumu wake, tukaweze kuwapata watu ambao ni viongozi wa makanisa, ili kuwatia ndani ya bunge wakaweze kusema ule ukweli ambao unafichwa kusije kukawa kuna siri za kuuwana na kushambuliana kwa kutafuta madaraka zaidi. Nafikiria hapo tutaendelea zaidi.

**Com. Mohammed Swazuri:** Nafikiri tunarudia rudia yale ambayo tumesema kwa hivyo hakuna maneno mapya ambayo tumeyasikia. Upande wa serikali ya majimbo kama vile nimeshaeleza, upande wa elimu mwalimu ameeleza hapa tunataka national syllabus halafu tuwe na syllabus za mikoa. Powers zimepewa kwa hizo serikali za mitaa kuamua zitafanya vipi mambo yao ya elimu, sio elimu pekee yake ni mambo yote. Elimu, afya, barabara kila kitu ziko katika powers za mikoa hapo.

Halafu revenue ile ambayo inapatikana, mapato yanapatikana yawekwe kwa sehemu kubwa iende kwa mkoa, hiyo tayari iko. Utalii College nafikiri tulikuwa na mipango ya kujenga Utalii College hapa, sijui mipango hiyo imefika wapi na uwajiri wa kazi kama nimesema pale pale ni wa district ndio itaajiri. Kwa hivyo hao wenyewe watashindwa wenyewe.

Halafu mambo ya maji. Tumesema hapa kwamba ni haki ya kupata maji sasa ni haki ambayo ni lazima itekelezwe na serikali.

Kwa hivyo sasa serikali ipitishe sheria au ifanye mipango yake ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata hizi hudumma kama inavyotakikana katika sheria. Kwa hiyo itakuwa sasa hio mipango unayosema mzee kuhusu mambo ya maji na sehemu zile kame tumeshaeleza hapa kwamba itabidi serikali sasa ifanye mambo yake kama inavyotakikana. Haya naona kwa vile watu wanarudia rudia sijui nianze na nani ambaye, maanake nitawapatia nafasi moja moja tu. Maanake naona tunarudia yale yale tuliyosema. Haya.

**Mohammed Sharif Omar:** Katika haya maswala hapa tumegusia kuhusu crown land na ukatujibu kuhusu crown land. Ukasema kuwa serikali bado inatizama. Lakini sisi tulikuwa tunaomba hivi kwa sababu wajua sehemu za kwetu, mimi in fact kuhusu crown land za Mazurui mimi nazielewa vizuri kutoka background zao kwa sababu mimi naishi nao kule. Kuna tension ambayo inaendelea saa hii, bado hakujatokea vita mpaka sasa lakini kuna maneno ambayo mabaya mabaya yanatokea. Kwa sababau Mazurui kwanza walipopokonywa ardhi na serikali, walijua kua wamepokonywa, kisha baadaye wakashtaki. Sasa zile ardhi zimegawanyiwa watu, zote zimegawanyiwa watu. Kuna watu tayari wamegawanyiwa, wamepewa numbers na kuna wengine saa hii bado wanaendelea kudhulumiana dhulumiana. Mtu anaandikishwa jina akienda offisi kule anaona jina limebadilishwa. Sasa ikiwa serikali itaendelea kuchunguza hii mamba na hii mambo hata hawa crown land wamekuja kunyakua. Kwa hivyo Katiba na sisi raia tuna haki tuki-declare kwa serikali kuwa Katiba imesema crown land zitachukuliwa na serikali. Serikali zile sehemu ambazo zimegawanyiwa raia mpaka dakika hii, kuna wengine wanachimba mawe kule. Kulikuwa na Muitaliano mmoja ambaye yuko Boja saa hii, Cascroblocks, alikuwa Takaungu na aliondoshwa wakati kulikuwa kuna kesi ya Mazurui wanaendeleza kwa korti, ikatolewa barua ya koti aje aondoshwe ule kwa sababu wanasema kuwa Mazurua bado wana ile tamaa kuwa ile ardhi ni yao, bado hawajalipwa kitu. Lakini wanatarajia kulipwa na serikali kitu gani? Hakuna haja ya kulipwa kitu kwa sababu hawa watu ni wazaliwa pia wa pale. Hao Mazurui wenyewe waliokuja walikuja zamani sana. Wale watu walioko pale, ukisikia Mazurui, nafikiri pengine watu wakisikia Mazurui wanasikia ni Mwarabu, wakiona mtu kama huyu wanasema ni Mazurui. Lakini Mazurui ni watu kama nyinyi tu. Ni watu ambao ni black, wazazi wao ni wakaumma, wazazi wao ni Mijikenda, Wagiriama. Sasa hawa wazee wamekwenda kitambo. Wao wamepokonywa zile ardhi wamepokonywa, bado still wanunua mashamba mengine.

**Com. Mohammed Swazuri:** Haya, tunaelewa hiyo.

**Mohamed Sharrif Omar:** Sasa hii Katiba ilazimishe crown land zisichukuliwe na serikali, hiyo ndio naomba tu. Maanake sasa tension, watu watateta bure wakisema serikali bado inachunguza chunguza. Mohammed Sharrif Omar.

**Joyce Nduku:** Kwa jina ninaitwa Joyce Nduku na ninasimama hapa mbele ya hii Tume ya Kurekebisha Katiba. Kwanza ninawarudishia asante na shukrani. Jambo la kwanza ambayo ningetaka hii macommissioners wale wanasikia maoni, hapa ninafikiri akina mama ndio wengi zaidi na sijui ni kwa sababu gani hakukuruhusiwa akina mama waongee kwa Kigiriama halafu ikatafsiriwa kwa sababu…..

**Com. Mohammed Swazuri:** Hatujawakataza mama, nimeuliza akina mama kuna mtu (inaudible) mara nyingi sana.

(inaudible) Kumetokea mtu moja akasema anaongea kwa niaba yao.

**Joyce Nduku:** Haya mimi nimejitokezea ninataka akina mama wale ambao wako hapa waongee kwa sababu wako na shida nyingi.

**Com. Mohammed Swazuri:** Waambie wewe basi waongee.

**Joyce Nduku:** Akina mama ninawaomba wale nyinyi mko hapa kwa sababu sisi ni wengi kuliko hao wanaume na nina hakika nyinyi ndio mko na shida nyingi zile tunakabidhiwa huko manyumbani. Kwa hivyo ninawaomba muulize maswali hata kama ni Kigiriama, kuna watu wa kutafsiri, si ndio. Haya.

**Com. Mohammed Swazuri:** (inaudible)

**Audience:** (inaudible)

**Joyce Nduku:** Swali la kwanza ile ninataka kuuliza wale ambao wako mbele yetu, isipokuwa tu hawakuleta public address system. Hii ni kitu muhimu sana ambayo ingeletewa public address system kwa sababu inahusu maisha yetu. Kwa hivyo wakati ule mwingine mnaenda huko vijijini, ni vizuri mkawa na public address system. Kwa sababu maswali inakuwa addressed kwa hiyo meza na wale tuko kule nyumma hatusikii zingine.

Swali langu la kwanza macommissioners wale ambao wameenda kusikia hii marekebisho ya Katiba, ninataka kuuliza mmeenda kama mmegawana. Tunasoma kwa magazeti mko groups mbili. Na mmegawana nyinyi wenyewe, itakuaje? Sasa yale maoni mnaenda kusikiza kwa wananchi ambao group ingine ambao tunasikia hamsikizani, ambao watu hawataandika ile vitu zao ambao wanafikiria. Kwa hivyo hapo ninauliza macommissioners mko mara mbili kwa hivyo hiyo ni neno moja.

Swali lile lingine ninataka kuongea ni afya bora. Afya bora imesemekana katika ile Katiba mpya kila mwananchi ako na haki ya afya bora. Halafu hii Katiba mpya sijui vile itawezekana kupatia mwananchi wa kawaida matibabu ya bure kwa sababu wananchi wale wengi ndio wanaishi vijijini. Na mahospitali nyingi ni za cost sharing, na huyu mwananch ambao ako hapa hawezi akapata Shilingi kumi ambazo ni za cost sharing. Itawezekanaje hawa watapata namna gani hizo pesa na mnasema atapatiwa matibabu ya bure na hii kuhusu katika hii haki ya afya?

Ya tatu nataka kuuliza ambao inatuhusu wafanyi kazi wa serikali. Wafanyi kazi wa serikali wale tuna-contribute pesa za NHIF. Hawa wafanyi kazi wana-contribute hizo miaka kwa miaka hamsini na tano. Miaka hamsini na tano kwa bahati nzuri sikugonjeka. Na nikiangalia hivi nyumma yangu, hao watu wote walikuwa wafanyi kazi wa serikali siku moja. Na wali-contribute hizo pesa kwa miaka hamsini na tano. Bahati mzuri hawakulala hospitali. Je, akienda nyumbani ambao anahitaji

zile miaka za uzeeni, akihitaji hizi pesa za hospitalini pengine anataka hio matibabu ndio hatapata matibabu ya bure. Na yet ali-contribute hizo pesa katika miaka hamsini na tano. Tunataka hio mambo iangaliwe kwa wale watu wanastaafu ndio wengi huko manyumbani.

La tatu pia ninataka kuongea pia ni NSSF. Hiyo Social Security Number hizo tunaona kwa NSSF. Hizi pesa wafanyi kazi wa serikali kusema kweli wanatoa kila mwaka halafu hizi pesa zinaenda zinawekwa kwa mabanki. Mabanki hizo ndizo zinaanza kukopesha. Halafu mwenye alitoa mfanyi kazi wa serikali hawezi akapata hata mkopo katika hizo pesa. Tungetaka at least na investments, kusema kweli investments tumeona ni wrong investments, ile serikali inaenda kuingia katika hizo investment ambazo sio za kawaida. Kwa hivyo mfanyi kazi ule ame-contribute hizi pesa mwaka wa hamsini na tano hakuna kitu ambacho anafaidika. Zinaenda kufaidi wafanyi biashara wengine ambao wanaenda kuomba hizo pesa katika banki. Kwa hivyo kwanza ninataka kufikia hapo, nitaendelea na kuuliza baadaye. Asante.

**Kamtu Karisa:** Asante kwa kupata nafasi hii. Jina langu naitwa Kamtu Karisa kutoka Petanguo. Mimi basi maoni yangu ni zile kama tunavyony’any’aswa watu wa Pwani. Watu wa Pwani wanay’any’aswa sana na watu wa bara hata wakiwa kuna kazi imetokea, watoto wa Pwani wakifika wanaambiwa kazi imeisha watu wamepatikana tayari. Hata hakuna mtoto ambaye atapata kazi pengine ni wawili, watatu lakini watu wa bara ndio watapata kazi. Kwa hivyo tunaona Kenya ni mmoja na uhuru tumepata kila mtu anaambiwa kuna uhuru lakini uhuru tunaona uko upande mmoja, upande wa Pwani hakuna uhuru. Watu wa huku basi wanapata shida sana kwa vile watoto wa Pwani wanadharauliwa hata watu wa Pwani wanadharauliwa na tunaona sisi ndio watu wa Pwani. Na kule kwao hawataki watu wa bara wanapenda Pwani lakini wakifika hapa basi wanadharau watu wa Pwani. Basi tunaona uchungu ikiwa ni maoni inatokea ni lazima kila mtu ajulikane kama ni raia wa hapa Kenya. Sio kupendelea watu wa bara watu wa Pwani wanadharauliwa. Tunasikia uchungu hata kama wale walisema hakuna majimbo lakini ikiwa hakuna majimbo lakini tuwe pamoja. Sio watu wa Pwani kudharauliwa watu wa bara ndio wanaendelea. Basi tunasikia uchungu, hata watoto wadogo ambao wanaenda shule. Kuliambiwa watoto wa nursery wataenda bure. Hata mtoto mdogo wa nursery lazima umtolee mia mbili ndio aanze masomo. Sasa sisi watu wa Pwani hata tukiwa maskini, tutasomesha wapi watoto wetu na vile ukiwa kama ni mama pengine amefiwa hana bwana. Na akiwa nursery yenyewe itakuwa mia mbili, huyo mtoto atasoma namna gani? Basi sisi tunataka watu wa Pwani tuwe pamoja na watu wa bara. Ikiwa ni uhuru umepatikana umepatikana kila pahali isiwe uhuru wa pahali pamoja. Mimi natoa maoni hiyo ikiwa ni kawaida itatoka basi itokee tuwe tunakuwa pamoja tusidharauliwe watu wa Pwani. Hayo ni basi Mungu awabariki.

**Com. Mohammed Swazuri:** Akina mama wengine. Msione haya. Jina lake kwanza.

**Bahati Charo:** Jina langu naitwa Bahati Charo

**Translator:** Jina lake anaitwa Bahati Charo.

**Bahati Charo:** (Vernacular)

**Translator:** Shida yangu iliyonifikisha hapa ni kwamba,

**Bahati Charo:** (Vernacular)

**Translator:** Nafunza mtoto.

**Bahati Charo:** (Vernacular)

**Translator:** Sasa anamaliza darasa la nane.

**Bahati Charo:** (Vernacular)

**Translator:** Nimetafuta pesa,

**Bahati Charo:** (Vernacular)

**Translator:** nimepeleka kwa mwalimu,

**Bahati Charo:** (Vernacular)

**Translator:** halafu mwalimu amegoma.

**Bahati Charo:** (Vernacular)

**Translator:** Zile pesa nilizopeana kabla hajagoma na sasa amegoma, wakati mwalimu akirudi, nitaenda nipeane pesa nyingine ama ni hizo hizo nilizolipa hapo nyumma kabla alikuwa hajagoma?

**Bahati Charo:** (Vernacular)

**Translator:** Hilo ndilo swali langu lililonifikisha hapa.

**Bahati Charo:** (Vernacular)

**Translator:** Sina mengi.

**Jumwa John:** Kwa majina yangu naitwa Jumwa John. Swala ambalo nauliza mimi ni kwamba kuna mambo yale ya pension. Mimi bwana wangu alifariki mwaka wa themanini na nane. Ikiwa nimepata zile pesa za cooperative nikasomesha watoto zikamalizika. Ukaja zile ambazo ni za mwezi ambazo ninachukua nusu nusu kila mwezi. Nilienda hata nikafikisha miezi sita. Nikifika huko ikawa zile cheque ziliandikwa kweli jina lakini pesa hazikuandikwa, hazijulikani ni ngapi. Ikawa kila mwezi zikija huwa nazirudisha kwa DC maanake tuliambiwa turudishe huko halafu zikapelekwa Nairobi tupate majibu. Basi ilikuwa kila mwezi ikitoka mimi huwa napeleka huko mpaka sasa. Wakasema basi mama hivi pengine computer imekosea kwa hivyo nenda ukakae halafu utakuja tena. Nikakaa mpaka leo hizo pesa ambazo nilikuwa nichukue kila mwezi zijazipata mpaka leo. Kila nikienda wanasema mama nenda ukatulie, tutaandika barua tupeleke mpaka sasa hatujazipata. Ni kwa nini hazijatoka

mpaka sasa au vile walivyoniambia kuwa, niendelee na kusomesha wanangu na zile pesa nitazipata hizi ambazo hazitoki, nitawasomesha na nini? Nataka nijue kama hazitatoka kabisa, zimeenda wapi? Kwa maana mara ya kwanza walinielezea kuwa ziko na sasa hazitoki, karatasi niko nazo na sipati chochote. Nataka nielewe ni kwa nini hazitoki.

Swala la pili ni kwamba upande wa wamama. Wamama wamejitolea sana kuwa na vikundi vya wamama. Tunataka faida tupate pale kwenye vikundi vyetu. Kwa sababu gani tukiwa pengine kama ni mfereji au ni upande mwingine, haswa mfereji. Tunatoa pesa huku kunatoka maji? Ni wakati tu mara maji hayatoki. Zile siku tunauliza kwanza zile siku ambazo hazitoki maji, zinaandikwa na ile meter ama haziandikwi? Na kama haziandikwi ni kwa nini leo nikapeleke pesa mwezi huu, kesho yake ama mwezi huo ujao niende tena? Nikifika bill ni elfu ishirini na mbili na mwezi uliokwisha mimi nimelipa? Nikiuliza naambiwa maji yamepitia hapa kwenye meter kwa hivyo ziliandikwa. Vyaandikwa vipi? Nataka nijue vimeandikwaje? Ikiwa mimi sijui zimeandikwaje. Na kama zimeandikwa mbona zinaandikwa zaidi na kila ninachopata ni kidogo? Wamama wanataka faida nao waendelee na vikundi vyao. Sio tuwe tunauza vitu halafu tupange faida ya kampuni. Hatutaki, wamama wanataka faida ili makundi yao yaendelee. Ni hayo Mungu awabariki.

**Morris Sifa Kahindi:** Mimi majina yangu naitwa Morris Sifa Kahindi. Ningependa tu kuzungumzia jambo moja. Jambo hili ningependa msikize kwa makini sana. Jambo hili ni kuhusu viongozi hasa hawa wa kuchaguliwa hawa. Katiba mpya inasema viongozi watachaguliwa kwa njia kijijini mpaka huko juu. Hiyo tunashukuru sana. Lakini, kuna hatari moja ambayo ningependa sote mnisikize kwa makini sana. Na ningependa Katiba hii mpya iwe itajumuisha mapendekezo haya ambayo nitatoa hapa.

Tukiangalia upande wa viongozi hawa wa kuchaguliwa, kwa miaka mingi sana viongozi wamekuwa wakinunua uongozi wao. Tumeona ya kwamba wale ambao hawana uwezo ama hawana pesa wengine ni viongozi wazuri kabisa lakini hawachaguliwi kwa sababu hawana pesa. Wale ambao wana pesa wengine si viongozi wazuri lakini wamechaguliwa kwa sababu ya zile pesa zao. Kwa hivyo tukichunguza sana tutapata ya kwamba ile shida ambazo tunalalamika leo ni kwa sababu tumechagua viongozi ambao ni wabaya. Tumechagua viongozi wale kwa sababu wana uwezo fulani.

**Com. Mohammed Swazuri:** Unapendekeza nini?

**Morris Sifa Kahindi:** Ningependekeza hivi basi. Bali na ile yakuwa watu watangaze msimamo wao au utajiri wao, wale viongozi, ningependekeza ya kwamba, viongozi wote wakichaguliwa wawe pia ni wazaliwa wa ile sehemu ambayo wanaongoza. Kwa sababu tumeona ya kwamba kunayo hatari ya kwamba mtu anawezapata mali nyingi huko hatujui ametoka wapi. Akifika sehemu fulani ambayo pengine mwenyewe amepanga atatetea kitu fulani huko cha uongozi, anadanganya wananchi na ile mali yake amepata kule, anashiriki kwenye miradi mingi ya maendeleo kama ni michango anatoa mikibwa mikibwa. Wananchi wanakuwa confused wanamchagua wanafikiri yule ndie kiongozi mzuri.

**Com. Mohammed Swazuri:** Mengine?

**Morris Sifa Kahindi:** Lakini ile background yake sasa hawaijui kule mahali ametoka.

**Com. Mohammed Swazuri:** Enda kwa nyingine hiyo niko nayo tayari.

**Morris Sifa Kahindi:** Hiyo moja tu, sina nyingine, bado naeleza tafadhali.

**Com. Mohammed Swazuri:** (inaudible)

**Morris Sifa Kahindi:** Tafadhali nataka kueleza kitu.

**Com. Mohammed Swazuri:** (inaudible) Mwingine.

**Morris Sifa Kahindi:** Ilikuwa ni hiyo tu lakini kuna mambo nilikuwa ninataka kueleza.

**Com. Mohammed Swazuri:** (inaudible)

**Daniel Baya:** Mimi naitwa Daniel Baya na nitasema machache nitasema mambo manne ambayo sikuyasikia yakizungumzwa hapa. La kwanza watu wengi wanapata ajali za magari, na ile insurance act vile iko proceedings sijui zinaenda vipi zinachukua miaka mingi, kitambo wawe compensated watakuwa wamekufa. Kwa hivyo Katiba hii inayokuja iangalie swali la insurance act. Mtu akipata ajali anapata pesa yake as soon as possible, within a period at least of six months or seven months. Na sikuwasikia mkilitaja neno hilo hapa.

La pili, tulipokuwa tunatoa maoni watu wa Ganze, niliwasikia wamama wakisema katika baada ya kilomita tano wanataka kuwe na maternity na dispensary. Ili akina mama idadi ya wanaokufa kabla ya kufika hospitali wawe watapata msaada. Akina mama jambo hilo sasa hivi wamelisahau. Mimi nilisoma mapendekezo yenu, na sasa nasema tume iangalie kama kipengele hicho hakikuangaliwa kikaangaliwe. At least huku vijijini ambapo watu hawana uwezo na hakuna magari. Katika baada ya kilomita tano au sita kuwe na dispensary na mahali akina mama wanaweza kujisaidia kuzaa.

Neno lingine kuna public servants wengi hapa. Wame-retire au bado wata-retire. Kabla wa-retire wanaletewa barua na PS kwamba wata-retire mwezi fulani wanashukuru kwa mda waliofanya kazi. Kufuata hizi pesa zao inachukua miaka kumi au ishirini. Ile retirement benefit act ya public servants iwe reviwed, ili mtu aki-retire, akiandikiwa barua na kushukuriwa na PS kabla a-retire iwe na cheque yake kabisa ya benefits zake na jambo hilo mmelisahau hamkuliongea hapa.

Lingine akina mama walitoa oni wakasema sisi tukiolewa tena tunataka kule kwa baba zetu tuwe tutapata share ya uridhi wetu

na hapa hamkuongea maneno hiyo. Katiba hiyo ijayo tunaomba akina mama hata kama ameolewa kule kwa baba yake awe na sehemu ya mali fulani atakayoiridhi kama yake. Asanteni.

**Timothy Kalume:** Kwa majina ni Timothy Kalume. Nina oni moja tu. Na oni hilo hasa litahusu upande wa shirika ya world health organization ambayo ilileta mpango wa madawa hii ya lymphatic pylariasis. Katika sehemu ya location hii ya Ganze, tulipata mafundisho na tukaendeleza hizo dawa vijijini lakini hali ya kimalipo tulipouliza ule wakati wa seminar hatukuambiwa tutalipa kwa kiasi gani. Sasa tunaomba ule ufisadi ambao unafanyika humo maofisini humo kutoelezwa ule uwazi wa kuwa mnafanya hivi lakini mtalipa kiasi kadhaa, ninaomba hii tume hali namna hiyo iweze kuangalia sana. Maanake tuliambiwa tunalipwa shilingi mia nane, huku tunasikia ni elfu nane kwa kila mmoja na ni shughuli kubwa sana ambayo ilifanyika. Tafadhali tume iangalie hiyo mambo.

**Com. Mohammed Swazuri:** Isiwe unarudia tafadhali maanake sasa tunaenda kwa mambo ambayo sio ya Katiba. Ni mambo ambayo ni sheria ndogo ndogo. Haya last person, wewe utakuwa mtu wa mwisho.

**Kiboni Kiraga:** Mimi kwa majina naitwa Kiboni Kiraga na ninashukuru sana tume kwa kutilia mkazo elimu ya malezi pamoja na elimu ya msingi. Lakini sasa kuna swala moja ambalo pia ningependa tume iweze kuliangalia. Kwa sababu utakuta kwamba wanafunzi wote ambao wataenda darasa la kwanza mpaka la nane, sio wote wataenda secondary ama shule ya upili. Lakini unakuta kwamba, pale haikuelezwa kama mwanafunzi hakufanya vizuri kuenda secondary. Je, ataenda wapi? Haikuelezwa hapa katika Katiba mpya. Kwa hivyo mimi ilikuwa maoni yangu nasema, tume ya marekebisho ya Katiba iweze kutilia mkazo mafundisho au vyuo hii vya ufundi. Kuweze kujengwa kila lokasheni ipate chuo kimoja cha ufundi na kipatiwe vifaa vya kutosha ili wanafunzi wote ambao hawataenda shule za upili waweze kupata mafundisho pale ili waweze kujifundisha kazi na baada ya mda, waweze kujiajiri wenyewe. Kwa hivyo hayo ndio yalikuwa ni maoni yangu.

**Com. Mohammed Swazuri:** Kuna swala moja la….tuanze na huku mwanzo. Crown lands ya Mazurui nafikiri tumesema mambo yake hayo. Tumesema kwamba sheria itaangalia matatizo ya hizi crown lands, mikataba ya zile Mazurui za akina nani, zote zitaangaliwa. Hiyo sijui nirudie mara ngapi. Itaangaliwa na nimesema ikiwa kutachunguzwa ikiwa mtu alichukua ardhi kwa njia ambayo haifai, uchunguzi utabainika either kama ni kupokonywa ardhi au ni kulipa fidia kwa wale wenyewe au ni kuregeshewa wenyewe au irudi kwa serikali, national land commission itaangalia hio. Tumesema kwamba tutaenda nyumma kadiri tunavyoweza. Kama ni mwaka elfu moja, mwaka mia nane na tisa mpaka tujue hapo itakuwaje. Sidhani kama naweza kueleza zaidi ya hapo.

Halafu mama Joyce habari ya public address scheme, hiyo tumesikia. Halafu akasema kwamba wanatume wamegawanyika. Kwa kweli ile reporti ambayo mliiona jana imetushangaza hata sisi kwenye magazeti. Kwa sababu tofauti yetu kubwa iliyoko ni tofauti ya mawazo. Na katika watu ishirini na saba hutazamii kwamba wote watakuwa na mawazi sawa. Basi ingekuwa si tume hiyo. Watu huwa tunashindana, tunapingana lakini mwisho sote tunaelewana. Na hiyo ndio kawaida hata bunge pia ni

hivyo. Wao wabunge wanapingana lakini mwisho lazima patoke sheria ya watu wote wakubaliane. Basi kama ni kura kama ni nini, hiyo inakuwa hivyo. Mimi nime-participate katika kila stage ya hii review commission. Katika kuandika ile draft na hakuna siku au session yoyote ambayo nimekosa. Lakini nakuhakikishia kwamba hakuna neno ambalo tumeliandika hapa ambalo tulipiga kura, hakuna, hakuna kabisa. Mimi sikukosa hata siku moja. Lakini hakuna kipengele ambacho tumeandika hapa tukakosana sana mpaka ikawa, okay wale ambao wanasema tuandike ardhi ni hivi ni wangapi, wale wanaosema ni hivyo hakuna. Ilikuwa ni maelewano, concesus. Sasa hio division inayosemwa sijui yatoka wapi. Lakini tumezoea sisi katika hii tume vita huwa twapigwa vita vilivyomo visivyokuwemo, twatiliwa lakini sisi tumesema twaendelea na kazi yetu mpaka tummalize.

Halafu free health. Tumesema upande wa umeuliza mambo upande wa hospitali, madawa bure nani atatekeleza. Tumeweka sheria tayari hapa. Nimesema hizi rights hizi haki za kimsingi tumezitoa halafu tumetoa na obligation. Kwamba ni lazima ziwe obligated by the government.

NHIF na NSSF. Kuna retirement benefits act hiyo ni mpya na haya maswala uliyoyazugumza yote inaelezea. Kwa mfano upande wa investments wa hizi pension funds, ile retirement benefit act imeeleza vizuri sana kwamba ni lazima waweke kiwango fulani kwa property, kiwango fulani kwa biashara hili kiwango fulani kwa hivyo maswala ya NSSF sasa kidogo yamekuwa yanatatuliwa.

Mama amesema kuhusu madharau ya watu wa bara kuhusu watu wa Pwani nafikiri tumesema tunaunda taifa jipya lenye misingi ya kidemokrasia. Ikiwa utafuata sheria hii mpya tunayosema, imesema hatutaki kubaguana kwa aina yoyote pamoja na kubaguana kimikoa. Kwa hiyo itakuwa sasa mtu akifanya hivyo wewe una haki ya kumsomea hii sehemu ukamwambia hivyo unavyofanya wanidharau mimi mtu wa Pwani lakini Katiba imesema Wakenya wote wako sawa, hiyo tumeiandika.

Halafu mama amesema anauliza kama zile pesa alizolipa kabla ya mgomo ni zile zile au itabidi alipe nyingine waalimu wakirudi shule. Nafikiri jibu lake inaeleweka ambalo hutalipa tena. Waliogoma ni waalimu sio wewe, wewe ushalipa pesa zako.

Na mwingine matatizo yake ya pension, nafikiri hiyo ni problem ya ile ofisi inayo-deal na hii ni maswala ambayo yanaweza kutatuliwa either ni DO au DC--0

Lakini tumesema kwamba hapa sisi tunatengeneza broad principles. Kuna zile sheria ambazo siko tayari zinafanya kazi. Tutaangalia vile watu wanavyosema tupendekeze. Lakini kuna mambo ambayo lazima iingie kwenye Katiba. Yale mambo ambayo hatuwezi kuyatia kwenye Katiba lakini wananchi wameyasema, tuna sehemu hapa tumeiita transitional requirement or section. Tutaandika kwamba watu walisema kuhusu mambo ya ajali ni nyingi na insurance hawalipi kwa hivyo angalieni insurance act. Na tumesema mambo haya yote yafanyinke katika miaka hii miwili. Yote ambayo wananchi wamesema.

Maternity na dispensary kila five kilometers. Hiyo sasa itakuwa ni kazi ya ile serikali ya wilaya. Imepewa majukumu ya kupatia hudumma wananchi karibu kabisa inavyowezekana. Sasa wakishindwa watakuwa ni wenyewe wa wilaya lakini sio Katiba. Katiba imewapatia ruhusa ya kufanya hivi.

Halafu kuna swala la retirement nimetaja hilo. Halafu mzee akasema Daniel kwamba msichana au mwanamke aliyeolewa awe aweza kuridhi ardhi ya kule alipozaliwa. Sasa sijui atarithi kule alikoolewa nako au ni huko kumoja. Manaake isiwe ile argument ya marriage ni kwamba kule anakoolewa, yeye naye atakuwa ni shareholder kule. Si unaona ni hivyo au sio hivyo? Mwanamke anarithi kule anakoolewa. Lakini sasa wewe wasema kwamba yeye ameolewa arithi kule halafu tena huku kwa baba yake pia, kwa mila nyingi akiondoka kule akirudi nyumbani basi, yeye ni mtu wa pale ana haki yake. Lakini kama ameolewa huko miaka sabini amekaa kwa bwana wake, nafikiri mila nyingi zinasema kwamba huku hana chake tena. Tumeiweka wazi tumesema kwamba sasa itategemea dini na mila ya wale watu lakini tu mtu asithulumiwe. Hawezi kukaa kule akarudi hapa nyumbani mkasema wewe file yako ilikuwa tumeiondoa shauri yako. Akirudi ni mtoto wa pale pale atarithi lakini kama atakufia huku kwa bwana wake, sasa huku sijui yuwafuata nini tena. Lakini ni maoni pia tunasikiliza.

Bwana Kibaga akauliza habari ya secondary school nani wataenda pale, nafikiri ni sheria ambazo ziko tayari hakuna haja ya kubadilisha. Mwanafunzi akimaliza standard eight ni aende secondary school.

**Interjection:** Na hata vyuo vya ufundi.

**Com. Mohammed Swazuri:** Ee vyuo vya ufundi viko lakini kwenye education act ziko, tayari hiyo sheria iko. Nikutekeleza tu ndio hatutekelezi lakini sheria iko. Haya nafikiri sasa tutafunga na kwa kweli tunasema tunawashukuru sana maanake watu wamekuja kwa wingi, Bwana coordinator kama yawezekana hawa akina mama wawekee mkutano wao maanake wajua mimi mila za hapa nazijua. Si rahisi sana hawa akina mama kuzungumza mbele ya wazee. Kwa hivyo siku nyingine ukiwa na viongozi wa akina mama kama vile akina mama Joyce, uwaite hawa, uwasomee, uwazungumzie ile Katiba vile ilivyoandikwa uwaulize maoni yao nao maanake sidhani kama wana uhuru wa kusema mbele ya wazee. Hii ni mila ambayo kila mahali tumeiona namna hiyo. Kwa hivyo akina mama mtapatiwa nafasi yenu na nyinyi mueleze vile mnavyotaka. Tumefanya hivyo sehemu nyingi ambao tumeona tumekwenda kuchukua maoni akina mama wananyamaza, tunamaliza, kama hivi wazee wanaenda zao, tunabakia wao wanasema kuliko wale wazee walivyosema. Kwa hivyo mtapatiwa nafasi yenu. Na kwa hayo machache tunawashukuru sana na tunashukuru sana kwa kutuunga mkono. Nafikiri Bwana Mwaringa atawaeleza kuhusu ile yellow ribbon aliyokuja nayo, lakini nyinyi maoni yangu ni kwamba, na naonelea na napenda sana wananchi wakijitokeza kwa wingi hivi, hii ni Katiba yenu, mmechangia mna haki ya kusema mnavyotaka kuhusu hii Katiba hii, mna haki ya kulilia ni nani ataitekeleza vile tunavyotaka. Kazi yetu tumefanya, mna haki ya kutuambia tumefanya vizuri au tumefanya vibaya, hayo ndio majadiliano ambayo tunayataka na tunawapongeza kwa hayo na tunawaomba muendelee kujitokeza zaidi katika mijadala hii. Asanteni sana.

**District Coordinator – Mwaringa:** Sasa nafikiri tumefika kilele lakini kabla hatujamaliza, kuna mambo mawili ambayo tutazungumzia. Kwanza kabisa nataka nimshukuru Commissioner wetu vile alivyoweza kutuelezea na pia nataka niwashukuru nyote kwa vile mlivyochangia. Na kama alivyosema Commissioner, huu ni mwanzo. Tutakuja tena na nataka niwahakikishie kwamba nitaanza tena na akina mama, nyinyi akina baba siwataki kuanza. Nitakuja kuzungumza na hawa akina mama kwanza. Kwa hivyo tutapanga pamoja na Councillor Susan Bire ambaye ni member CCC na hata wale akina baba wengine ambao wako katika hii committee pia sitawataka wakati huo. Nataka tukae, tuzungumze akina mama nao niwasikie. Halafu akina baba je na sisi tukutane pekee yetu? Mwatakaje na nyinyi? Hakuna wasiwasi. Lakini kwa ujumla nataka pia ku-acknowledge presence ya Bwana DO Joseph Sawe yuko hapa na pia nitamkaribisha katika ile hali ya kumaliza, ili azungumze na watu wake wa eneo hili, atatuambia mawili machache au matatu hivi na pia tuweze kufunga mkutano. Lakini kabla sijafika hapo, nafikiri maneno ya Katiba tumeelezewa na pengine yametukolea vilivyo na tumesikia wengine wakisema kwamba pengine wangependa uchaguzi ujao uwe katika Katiba mpya. Hayo ni maoni yenu sisi hatulazimishi mtu ni vile mnavyopenda nyinyi na viongozi wenu kama alivyosema Commissioner, ni sawa?

**Audience:** Sawa

**District Coordinator – Mwaringa:** Sasa hapa tuko na hizi tunaziita yellow ribbons. Pengine mmewahi kuona watu wakivaa yellow ribbons hizi ama ribbons za rangi ya manjano. (Vernacular) Hivi ni vitambara vya kummaanisha kwamba una haja na hamu ya kutaka Katiba mpya. Kwa hivyo kila unapokwenda unapotembea unaona nimevaa yangu. Hii ni kummaanisha mimi nina-support Katiba hii na ningetaka Katiba hii kwa sababu Katiba hii ni yangu nimechangia mwenyewe ndio maana ya kitambara hiki. Unapovaa kidude hiki hufungwi, hushtakiwi. Nikuonyesha tu ule msimamo wako kulingana na Katiba ambayo vile unavyoitaka wewe. Kwa hivyo msije mkahofu, mkasema Bwana tumepewa hivi. Hivi ni vitambara tunatoa katika jamuhuri yote. Popote pale tumeanza shughuli hii kutoka jana na popote pale utakapotembelea sehemu ingine utaona wananchi wamevaa vidude hivi kummaanisha kwamba tunapendelea Katiba mpya na iwezekanavyo hiyo ndio Katiba ambayo tunaitaka sisi kwa hivyo ndio maana yake. Una hiari ya kuchukua una hiari ya kukikataa kidude hiki, sawa. Hulazimishwi kwa hivyo tutasaidiana na wenzangu hapa baadaye. Tunataka utaratibu tukimaliza kufunga mtulie hivo hivyo. Wale wataweza kupata sawa, ambao hawataweza kupata msijali siku nyingine tukija tutakuja navyo lakini tunataka kuwe na hali ya utulivu ili tusiweze kuumizana lakini hiyo ni baada ya mkutano umefungwa, ni baada tumefanya maombi halafu ndio tuingie katika shughuli hii. Halafu mikutano mingine mtajua itakuwa lini, tutapanga na ile kamati yetu ya sehemu ya uwakilishini bungeni ya Ganze. Kwa hivyo nitamuita Bwana DO Joseph Sawe ili tafadhali uje uzungumze na pia utoe vote of thanks kwa tume na wageni wengine wote waliofika hapa. Bwana Sawe tafadhali.

**Joseph Sawe:** Basi asanteni sana, asante sana District Coordinator. Kwanza kabisa hamjambo wananchi?

**Audience:** Hatujambo.

**Joseph Sawe:** Leo ni siku kubwa kabisa ambaye tumeweza kuja hapa ili tuweze kusoma ile draft ambaye tayari imetoka, naona kila mtu karibu watu wengi wako nayo. Nataka kushukuru kwanza kabisa the commissioners kwa ile kazi ambaye tayari mmefanya kwa mda huo mfupi na leo tumeweza kuja hapa ili tuangalie hio kazi inapoanza. Nataka kushukuru ya pili wananchi kwa kuitikia mwito wa kuja hapa siku ya leo ingawa tulielezwa kwa mda mfupi kabisa lakini wengi wameweza kufika hapa, ingawa najua ya kwamba kuna wengi ambao hawakuweza kufika hapa na nashukuru vile umeweza kufika hapa na umesema mengi ambayo ya vile mlipata nafasi. Naona ya kwamba bwana Commissioner hao watu bado wako na mambo mengi wangependa kusema. Wengine hawajasoma hii draft, wengine hawajaelewa mambo yote ambayo iko hapa. Nataka kushukuru huyu Bwana District Coordinator kwa kusema ya kwamba una nafasi ambayo watu wataweza kujadiliana kuhusu hii draft zaidi. Basi wananchi mkiitwa, tukipanga tena na mkiitwa muweze kujitokeza na kutoa maoni zaidi kuhusu hio Katiba. Sina mengi nataka kushukuru kila mmoja sasa mwisho kwa kuweza kufika hapa na tukiitwa tuje tena Mungu awabariki. Asanteni.

**Speaker:** Haya, asanteni sana wageni wote ambao mmefika hapa. Hii ni location ya Ganze na langu ni kuwashukuru zaidi kwa hivyo tunaenda kilele ya mkutano huu ya kwamba mzee Shem Nyale atatufungia kwa maombi. Karibu mzee Shem.

**Shem Nyale: (Maombi):** Basi natuombe. Baba Mwenyezi Mungu Baba wetu wa mbinguni, mara nyingine tena tunakushukuru kama vile ambavyo Bwana umetulinda, umekuwa pamoja nasi katika mkutano huu. Tumeona Bwana maelewano ambayo Bwana umetuletea. Tumeona Bwana kila mmoja hakuridhika na yale ambaye ameyataja na yale ambayo ameambiwa. Na wakati huu Bwana tumekuwa wakati ambao tunakwenda kuachana. Tunawaombea wageni wetu hawa wote ambao Bwana wamekuja kutoka kule Kilifi, walinde Bwana wanaporudi kule sehemu za Kilifi na Mombasa pia Bwana tukijua ya kwamba nasi wananchi utatuacha hapa tukiwa na uzima. Bwana tunajua ya kwamba tutakutana tene hapa siku nzuri na ni siku ambayo Bwana tutakuwa na furaha kama leo. Twaamini umesikia katika jina la Yesu Kristo Mwokozi wetu. Amen. Asanteni.

Meeting ended at 2.00 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**